# Nipashe

Jumatatu Februari 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579844

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mke adaiwa kuua mumewe kwa kisu

UKURASA 3




UKURASA 13

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**BOSI MPYA TAMWA ATOA NENO KWA JPM**

MKURUGENZI mpya wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Rose Reuben, amemwomba...

UKURASA WA 11

**MSAKO MKALI WA POLISI MAUAJI YA MWENYEKITI**

POLISI mkoani Manyara, wanamshikilia mkulima na mkazi wa Kijiji cha Gijedabung, Limito Lebangu, (19), na kuendelea kuwasaka...

UKURASA WA 12

**DK. MENGI ATUNUKIWA TUZO HIFADHI MAZINGIRA**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi, ametunukiwa tuzo ya mafanikio katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira hasa kutokana na mchango wake alioutoa mkoani...


## UCHAGUZI TLS:

# Fatma Karume sasa atoa msimamo

UKURASA 2



Rais wa Chama cha Wanasheria nchini TLS anayemaliza muda wake, Fatma Karume.

## Wananchi Njombe waidokeza serikali

UKURASA 3

# Waziri awapa wiki polisi mauaji ya Mto wa Mbu

UKURASA 2


MICHEZO KILICHOIBEBA SIMBA, KUIANGAMIZA YANGA UK. 18

MAONI, KATUNI UK.6

# Vyama ushirika sasa vyasitisha shughuli kisa malipo korosho

**Na Lucy Ogutu,** MTWARA

VYAMA vya msingi vya ushirika (AMCOS) mkoani Mtwara, vimesitisha shughuli za ushirika kwa madai ya kucheleweshwa kulipwa fedha za ushuru Sh. 70 kwa kila kilo moja ya korosho, ambazo hutumika kuendesha shughuli za vyama hivyo katika msimu huu 2018/2019.

Wakizungumza na waandishi wa habari mjini Mtwara mwishoni mwa wiki, viongozi wa vyama hivyo kutoka wilaya tano, walisema malipo ya shilingi 70 kwa kilo moja ya korosho yako kisheria, hivyo kukosa malipo hayo mapema, vyama vimeshindwa kujiendesha.

Walisema ushuru huo umeshindwa kupatikana kupitia vyama hivyo kutokana na serikali kununua korosho na kutaka mkulima kulipwa fedha zake pasipo kukatwa na serikali kuahidi kulipa fedha hizo.

Hata hivyo, serikali katika kusimamia Sheria ya Vyama vya Ushirika, mwezi huu, imeanza kuingiza fedha hizo kwenye vyama vya msingi kwa kuanza na Sh. 14,000 kwa ajili ya kuwalipa makarani waliokuwa wanapokea korosho kwenye vyama ya msingi, wachukuzi waliokuwa wakipakia magunia ya korosho kutoka kwenye vyama vya msingi na kwenda kwenye maghala makuu na kulipa mishahara ya makatibu.

Shughuli zingine ambazo hazijaguswa na fedha hizo shilingi 14 ni pamoja vifaa vya ofisini, makatibu waliokuwa wanatumia gharama zao kutoka maeneo ya vijijini kuungana na timu za uhakiki maeneo ya mjini, lakini pia wajumbe waliokuwa wakutumika kusindikiza magari ya korosho kutoka kwenye vyama vya msingi vijijini kupeleka kwenye maghala makuu.

Kufuatia hali hiyo, wamesema ni ngumu kutoa fedha iliyoingizwa kwenye akaunti za vyama na kuwalipa watu waliotajwa kulipwa kwa sababu inaweza kuleta migogoro mikubwa na kuiomba serikali kuingiza shilingi 20 mapema ili watu wote wanaoguswa na malipo hayo waweze kulipwa, na baadaye wamalizie shilingi 36 zilizobaki.

Alipoulizwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Zizah Tumbo, hakuwa tayari kutoa maelezo kuhusiana na madai hayo.

Hata hivyo, alisema malalamiko hayo anayatambua na ameyawasilisha kwa Waziri wa Kilimo ili yaweze kufanyiwa kazi.

# Fatma Karume atoa msimamo uchaguzi TLS

**Na Enock Charles**

HATIMAYE Rais wa Chama cha Wanasheria (TLS), Fatma Karume (pichani), amefunguka na kutangaza rasmi kutowania tena nafasi hiyo.

Amesema sababu kubwa ya kutotaka kuomba nafasi ya kuendelea kukiongoza chama hicho ni washirika wake kumtaka kuwekeza muda zaidi katika shughuli zao.

Fatma ambaye anamaliza muda wake kuitumikia TLS Aprili mwaka huu, amekuwa kimya huku jina lake likikosekana kwenye orodha ya wanachama wa chama hicho walioјitosa kuomba nafasi za uongozi.

Muda wa mwisho wa kuomba nafasi za uongozi ndani ya chama hicho uliotolewa na kamati ya uchaguzi, utafika tamati Jumatano saa 11 jioni.

Fatma aliiambia Nipashe iliyotaka kufahamu kuhusu hatima yake ndani ya TLS kuwa, hatashiriki uchaguzi huo na kudokeza kusitikishwa na kauli iliyotolewa na mmoja wa viongozi wa mahakama nchini.

"Ni kweli sitoshiriki, 'my patners want me to dedicate my time to our business' (washirika wangu wanataka nitumie muda wangu katika biashara zetu)," Fatma alisema.

Alisema kuwa katika uongozi wake ndani ya chama hicho, amekumbana na changamoto nyingi, kubwa akiitaja kuwa ni kitendo cha mahakama kuchagua watu wa kufanya nao kazi.

"Hakuna kitu kilichonihuzunisha kama Jaji Mkuu kusema kwamba mahakama haiko tayari kufanya kazi na wanaharakati, sijawahi kusikia mahakama inachagua aina ya watu wa kufanya kazi nao," alisema.

Fatma aliongeza: "Akumbuke kwamba dunia imebadilishwa na wanaharakati na kuwa mwanaharakati ni jambo jema na si dhambi."

Fatma ambaye ni mtoto wa Rais wa zamani wa Zanzibar, alishinda kiti cha urais wa TLS Aprili 14, mwaka jana, akirithi mikoba ya Tundu Lissu.

Katika uchaguzi huo, Fatma aliwabwaga wapinzani wake Godwin Mwapongo, Godfrey Wasonga na Godwin Ngwilimi.

Fatma, ambaye katika uchaguzi wa mwaka jana alijitokeza katika dakika za mwishoni kugombea, ni rais wa kwanza mwanamke tangu kuanzishwa kwa kiti hicho mwaka 1954 kupitia Sheria ya Bunge ya mwaka 1954 (The Tanganyika Law Society Ordinance 1954).



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akikata utepe kufungua madarasa ya Shule ya Sekondari ya Matemwe, wakati wa ziara yake katika Mkoa wa Kaskazini Unguja Wilaya Kaskazini 'A'. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Waziri awapa wiki polisi mauaji ya Mto wa Mbu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ametoa wiki moja kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linafanya uchunguzi wa kina kwa kuwakamata watuhumiwa waliofanya matukio ya kikatili ya ubakaji na mauaji ya wanawake Mto wa Mbu wilayani Monduli, mkoani Arusha.

Akizungumza na wananchi wa Mji Mdogo wa Mto wa Mbu, jana kutokana na matukio hayo, Waziri Lugola alimwagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, kushirikiana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, na kusimamiwa na Mkuu wa Wilaya hiyo kuhakikisha uchunguzi wa kiintelijensia unafanyika juu ya watu wanaohusika kufanya vitendo hivyo vya kikatili katika eneo hilo.

Lugola aliongeza kuwa, haiwezekani wananchi wa eneo hilo wawe wanaishi kwa wasiwasi, wanateswa, kuuawa na kudhalilishwa wakati serikali ipo, polisi wapo, na wananchi wapo, kwa hatua hiyo lazima mauaji hayo yafikie kikomo.

"Ndugu wananchi serikali ya Rais Magufuli haiwezi kuchezewa hata kidogo, lazima tudhibiti hii taharuki, na tusipofanya hivi, hii hali itaendelea kushika kasi, jambo ambalo serikali haiwezi kukaa kimya," alisema Lugola na kuongeza:

"Kinamama wataisha kutokana na vitendo hivyo vya kikatili na lazima tuwe na uchungu sasa, Jeshi la Polisi lijipange vizuri kwa kufanya kazi ya weledi kwa muda wa wiki moja hakikisheni mnafanya kazi nzuri ipasavyo, ili kuwatia mbaroni hao watuhumiwa na kufunguliwa mashtaka haraka iwezekanavyo," alisema Lugola.

Lugola aliwatoa wasiwasi kinamama wa mji huo na kuwataka kutoa taarifa za siri kuhusiana na wahusika hao kwa sababu hawatoki mbali, bali katika mazingira hayo wanayoishi.

"Mmependekeza mpige kura za kimya kimya kwa kuwa uwanjani mkiandika majina ya watuhumiwa, mkipeleka taarifa kituo cha polisi kwa njia ya siri mnahofia mtakuja julikana, sijakataa njia mliopendekeza, lakini polisi watafanya kazi hii ya kiintelijensia hapa kwa umakini na watawakamata watuhumiwa," alisema Lugola.

Lugola pia aliwataka wananchi hao kutoa ushirikiano wa kina kwa polisi wakati wanafanya kazi zao. Pia aliwapa angalizo polisi hao wasije wakakurupuka wakati wanafanya uchunguzi huo, wasiwaonee wananchi, wahakikishe wanakuwa makini ili wasije wakawasumbua wananchi ambao wanafanya shughuli zao za biashara.

Mjumbe wa Kijiji cha Kigongoni, Kata ya Mto wa Mbu, Tarafa ya Manyara, wilayani humo, Devotha Steven, aliiomba serikali iongeze nguvu katika kuwalinda wanawake wa Mto wa Mbu kwa sababu vitendo vya kikatili dhidi yao vimekuwa vikiongezeka na kuwakosesha amani popote wanapofanya shughuli zao za kutafuta riziki.

"Mheshimiwa waziri, ninazungumza kwa machungu, kwanini tunateseka na serikali ipo, tunaamini mtasambaratisha haya mauaji, nasema kwa uchungu yatima wanaongezeka, tunaomba tupige kura na wananchi waitwe kutoka Tarafa ya Manyara na Makuyuni, ili wahusika wapatikane na tunaomba ulinzi utolewe kwa wale wananchi wanaotoa siri walindwe," alisema Devotha.

Mbunge wa Monduli, Julius Kalanga, alieleza kufurahia ujio wa waziri huyo, kumwomba jeshi lake liwakamate wahalifu hao ambao wanafanya vitendo vya kikatili.

## HABARI KITAIFA

# Mke matatani tuhuma kuua mume kwa kisu

**Na Waandishi Wetu**

MKAZI wa kitongoji cha Ukindo, Kijiji cha Lugalawa, Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, aliyetambulika kwa jina la Osmund Mwinuka, amefariki dunia kwa madai ya kuchomwa na kisu maeneo ya tumboni na mkewe, kwa sababu zinazoelezwa kuwa ni wivu wa kimapenzi.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, mmoja wa mashuhuda ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alidai kuwa mwanaume huyo ambaye ni fundi pikipiki na mkulima wa kijiji hicho, ambaye anakadiriwa kuwa na umri wa miaka (37), alichomwa kisu na mkewe akiyetambulika kwa jina la Anatoria Mtweve, majira ya jioni baada ya kurudi nyumbani akitokea kilabuni.

Shuhuda huyo alisema ugomvi wao unatokana na kile kinachodaiwa mwanamke kumtuhumu mumewe kumfuatilia nyendo zake za kimapenzi ikiwamo kwenye mitandao ya kijamii na njia nyingine.

"Yule mwanaume alipochomwa na kisu, alipelekwa hospitali ya misheni ya Lugarawa iliyopo kijijini hapo, lakini alifariki njiani kabla ya kufika hospitali," alisema shuhuda huyo.

"Ila usiku huo mwanamke alikamatwa na ilipofika majira ya asubuhi watoto wakubwa wawili walikamatwa na polisi kwenda kutoa ushahidi na mtoto mmoja alieleza kuwa baba na mama walikuwa wanagombana, ndipo mama akachukua kisu akamchoma baba akaenda kukiosha baada ya hapo akaenda kujificha," alidai shuhuda huyo akikariri maneno ya mtoto wa marehemu.

Naye Mwenyekiti wa kijiji hicho, Erasto Mhagama, alithitibisha kutokea tukio hilo na kuongeza kuwa ugomvi kati yao ulianza katika eneo la kilabu cha pombe za kienyeji kutokana na wivu wa mapenzi.

Alisema ni baada ya marehemu kumwambia mtuhumiwa kuwa ana uhusiano na wanaume wengine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Renata Mzinga, alithibitisha kupokea taarifa za tukio hilo, lakini alisema hawezi kutoa taarifa kwa sasa.

"Ni kweli taarifa hizi zipo, ila kwa sasa tunamaliza kwanza hili la watoto kuuawa kikatili, tukimaliza nitatoa taarifa juu ya hili," alisema Kamanda Mzinga.

Mtuhumiwa huyo anashikiliwa katika kituo cha polisi wilayani Ludewa, huku uchunguzi dhidi yake ukiendelea.

**Imeandikwa na Prosper Mfugale na George Tarimo, (Ludewa).**



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya mkopo uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.28 kwa Mrajis Msaidizi wa Ushirika mkoani Singida, Thomas Nyamba (wapili kulia) na Makamu Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Singida, Yahya Ramadhan (kulia). Watatu kulia mwenye miwani ni mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Augustino Matutu Chacha. Hafla hii ilifanyika mjini Itigi, mkoani Singida mwishoni mwa wiki.

# Samia aipa tano TADB kusaidia wakulima alizeti

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amepongeza juhudi za Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kusaidia wakulima wadogo nchini, hivyo kuongeza uzalishaji na kuwaongezea kipato.

Makamu wa Rais aliyasema hayo wakati akikabidhi hundi ya mfano yenye thamani ya shilingi bilioni 1.285 zilizotolewa na TADB kwa ajili ya miradi ya kilimo cha alizeti kwa wakulima 458 waliochini ya vyama vya ushirika (AMCOS) mkoani Singida.

Aliongeza kuwa wakulima waliopatiwa mkopo huo hawanabudi kuutumia katika kuongeza tija ya uzalishaji ili kufikia malengo ya mkopo huo ambao umelenga kuchagiza kusaidia sekta ya mbegu za mafuta ili kutanzua changamoto za ukosefu wa mafuta.

Aidha, Samia aliwaagiza viongozi wa ushirika mkoani Singida kusimamia kwa makini mkopo huo ili utumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kuhakikisha unarudi kwa wakati ili uwasaidie wakulima wengine.

"Nawashi muwe waaminifu kwa kuutumia mkopo huu vizuri na kuurudisha kwa wakati ili kuwawezesha wakulima wengine nchini waweze kukopeshwa ili kuchagiza uzalishaji wa mazao ya kilimo," aliongeza.

Mapema akizungumza na hadhara mjini Itigi ambapo mfano wa hundi hiyo ilipotolewa, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk,. Rehema Nchimbi, alisema mkopo huo utachagiza upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda 144 ya kusindika mafuta ya alizeti vilivyopo mkoani humo.

"Kwa kipekee tunaishukuru TADB kwa kutoa mkopo kwa AMCOS, mkopo ambao umelenga kuongeza tija ya uzalishaji wa alizeti hali itakayochangia upatikanaji wa malighafi ya uhakika ya viwanda

INAENDELEA UK. 8

# Wananchi Njombe waiomba serikali

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

WANANCHI mkoani Njombe wameiomba serikali kuwapa elimu juu ya kaya kuzingatia kukaa karibu kwa lengo la kuepuka vitendo vya utekaji na mauaji ya watoto pamoja na vitendo vyote vya kihalifu.

Ombi hilo lilitolewa jana wakati timu ya wataalamu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mkoa wa Njombe walipozitembelea familia zilizopoteza watoto kutokana na vitendo vya utekaji na mauaji ya watoto kwa lengo la kutoa pole na kutoa msaada wa huduma za kisaikolojia na kijamii.

Wakiwa katika familia ya Dau Ng'aala ya Kambarage Halmashauri ya Mji wa Njombe wilayani Njombe iliyopoteza mtoto wao, Oliver Ng'aala (5) aliyepotea Desemba 7, mwaka jana na kupatikana Desemba 8 akiwa amefariki.

Familia hiyo imesema kuwa suala la kaya kukaa mbalimbali imekuwa ni suala ambalo kwa sasa linatakiwa kufanyiwa kazi kwa sababu kukaa karibu kunaongeza usalama kwao.

Dau Ng'aala alishukuru Serikali ya Mkoa wa Njombe kwa kuwekea mkazo katika uchunguzi wa matukio ya utekaji na mauji ya watoto kwa kuwa yamesababisha huzuni kubwa kwa familia, mkoa wa Njombe na taifa kwa ujumla.

Aliongeza kuwa wao kama familia watatoa ushirikiano kwa vyombo vyote vya mamlaka katika kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa katika sehemu husika na sheria inafuata mkondo wake dhidi ya wote watakaobainika kuhusika katika vitendo hivyo vya kinyama.

Ofisa Ustawi wa Jamii Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Teresa Yomo, aliihakikishia ushirikiano familia ya Dau Ng'aala na familia zote zilizopatwa na matatizo kuwa atahakikisha wanapata msaada wa huduma za kisaikolojia na kijamii ili kurejea katika hali ya kawaida.

"Tupo pamoja na tutahakikisha mnapata msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa kuwa utawasaidia mrudi katika hali yenu ya kawaida kama zamani," alisema.

Kiongozi wa timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Hanifa Selengu, alisisitiza umoja na mshikamano katika familia wakati huu, huku wakiendelea na shughuli zao za kila siku za uzalishaji mali.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 22/02/2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Mtwara** kuelekea **Mbeya,** magari hayo yana namba za usajili:

**T221BYM/T887DJB**
**T636DFA/T837DJB**
**T133CCP/T574BZB**
**T296CZS/T900BAZ**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 27.0
Upana - mita 5.50
Kimo - mita 6.40

3. Njia itakayotumika: **Mtwara hadi Mbeya** Kupitia **Makambako,**
Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 06:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215065902

# Bosi mpya Tamwa atoa neno kwa JPM

Na Enock Charles

MKURUGENZI mpya wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Rose Reuben, amemwomba Rais John Magufuli, kutenga bajeti ya kimkakati kukabiliana na changamoto ya ukatili wa kijinsia unaozidi kushamiri nchini.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Reuben ambaye Januari 19, mwaka huu, alikabidhiwa mikoba ya Edda Sanga (amemaliza muda wake wa miaka mitatu) kukiongoza chama hicho, alisema kuna haja serikali kutenga fungu maalum kukabiliana na changamoto hiyo.

Aliipongeza serikali kwa kuanzisha dawati la jinsia ndani ya Jeshi la Polisi kukabiliana na ukatili wa kijinsia, lakini akasisitiza kuwa bila kuliwezesha, itakuwa ngumu kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mwandishi wa habari huyo mzoefu:

**SWALI:** Ukipata nafasi ya kuzungumza na Rais Magufuli kwa dakika mbili, utamwambia jambo gani la msingi?

**REUBEN:** Nikipata nafasi ya kuzungumza na Rais Magufuli, kwanza nitamshukuru kwa sababu vituo vya polisi vimekuwa na madawati ya jinsia.

Lakini pia nitamwomba kuwa, haya madawati yaimarishwe ili yaweze kufanya kazi yake vizuri ikiwa ni pamoja na kutengewa bajeti inayoweza kuwasaidia kufanya kazi zao vizuri.



Kaimu Mwenyekiti wa Tamwa, Judica Losai (kushoto), akimkabidhi katiba Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Tamwa, Rose Ruben, Januari 11 mwaka huu. **PICHA; MAKTABA**

Kazi ya dawati la jinsia si nyepesi maana pengine wanakuja watu wamepigwa, wameumia, watu waliolala njaa na kadhalika. Haya madawati yana changamoto nyingi.

Kwa hiyo, ningemwomba Rais katika haya madawati ayaongezee nguvu, yawe na bajeti ya kimkakati ili tuweze kupunguza matatizo ya ukatili wa kijinsia.

Lakini pia ningemkumbusha Mheshimiwa Rais kuwa huu ukatili wa kijinsia unapoongezeka, inakuwa shida kutekeleza sera yake ya 'Hapa Kazi Tu'. Hapa kazi tu inafanywa na mtu ambaye kwa namna yoyote ile haki yake imelindwa, ikiwa ni pamoja na kutengwa na ukatili wa kijinsia.

**SWALI:** Tamwa umeikuta inakabiliwa na changamoto ipi kubwa na unaitatuaje?

**REUBEN:** Tamwa kama shirika ambalo linategemea ufadhili, ni moja ya mashirika ambayo yanakabiliwa na changamoto kufanya kazi yake.

Ukiangalia masuala ya ukatili wa jinsia, masuala ya ukeketaji, mimba za utotoni, ndoa za utotoni, ni vitu ambavyo bado wimbi lake ni kubwa nchini.

Kwa hiyo, Tamwa ingetamani kuwa na jamii ambayo inaangalia na kuthamini haki za binadamu. Kulingana na ukiukwaji wa haki za binadamu katika eneo hilo, Tamwa bado ina changamoto kubwa.

Kwa hiyo, naweza kusema kuwa nimeikuta Tamwa ikiwa na changamoto kubwa ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia maeneo mengi mpaka kufika kule vijijini, bado wimbi ni kubwa.

Unaposikia idadi ya watoto kupotea imeongezeka, basi jua ya kwamba kuna ukatili wa kijinsia mahali fulani, unaposikia kuna wahamiaji haramu wamekamatwa mahali ama watu fulani wamepigwa, basi jua kuna ukatili mahali fulani.

Lakini changamoto nyingine ni katika suala la fedha. Tamwa haina chanzo cha pesa zaidi ya kutegemea kutoka kwa wafadhili, na wafadhili wengi fedha zao wanazielekeza katika malengo yao wanayoyatamani.

Kwa hiyo, ni changamoto nyingine kubwa lakini bado katika kile kidogo tutakachokipata, tutaendelea kukitumia. Tamwa tutaendelea kuhamasisha wafadhili wa ndani na nje ya nchi watambue kuwa nao ni sehemu ya jamii yetu, watuunge mkono kwa kutufadhili ili tuendelee kufanya kazi ya kupiga vita ukatili wa kijinsia.

**SWALI:** Umekiri ukatili wa kijinsia bado ni changamoto kubwa nchini, Tamwa ya Rose ina mkakati upi kukabiliana nao?

**REUBEN:** Kwanza nitaiendeleza tulipofikia kwa sababu kuondoka kwa Edda Sanga hakumaanishi kwamba tutaishia alipokuwa amefikia, hapana, nitaiendeleza vizuri na kwa makini sana ili kupate mafanikio makubwa zaidi.

Tunapaswa kushawishi kupata fedha kutoka kwa wafadhili wetu pamoja na jamii kwa ujumla kwa kutumia vyombo vya habari ambavyo vingine ni rafiki na vingine si rafiki katika kuufikia umma kupiga vita ukatili wa kijinsia.

Tunapoona kuwa ukatili wa kijinsia unaongezeka, vifo vinaongezeka, ni wananchi wale. Kwa hiyo, nguvu kazi inaondoka, idadi ya watu waliouana kwa sababu ya wivu wa mapenzi ama kwa kupigwa kwa sababu hakupika, watoto waliobakwa, hiyo ni nguvu kazi ya taifa ambalo mwisho wa siku tunahitaji kuwa na Watanzania ambao watatufikisha katika kuwa na Tanzania ya viwanda.

Tanzania ya viwanda haiwezi kupatikana kwa watu ambao wamebakwa, watu ambao wamepigwa na kuumizwa, inahitaji jamii ya watu wazuri ambao watafanya kazi vizuri.

Nitakachokifanya mimi ni kuendeleza kile kilichopo. Kuendeleza haya mapambano ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa sauti kubwa zaidi, tutatumia vyombo vya habari zaidi, tutatumia kalamu zetu zaidi kuielimisha jamii na kuipasha habari kuhusiana na masuala ya kijinsia.

Kwa waandishi wa habari, zile habari zinazoandikwa na kuishia katikati, sasa ziendelezwe.

Habari nyingi za ukatili wa kijinsia zinaandikwa halafu zinaishia katikati, zinaishia katikati eti ooh wameamua kwenda kukubaliana nyumbani ama ati wamesameheana, wamesameheana lakini ule ukatili uliofanyika bado ni kitendo cha kupigiwa kelele na umma.

**SWALI:** Kwa miaka takribani 30 tangu Tamwa ianzishwe, unafikiri lengo la kuwa na waandishi wengi wanawake kwenye vyombo vya habari nchini limefanikiwa?

**REUBEN:** Kuwa na waandishi wa habari wengi katika vyombo vya habari kama ilivyo lengo la Tamwa, naweza kusema kuwa limefanikiwa, lakini pia halijafanikiwa na pengine halijafanikiwa kwa sababu kazi ya uandishi wa habari ni utashi, kazi inayotakiwa uwe na bidii.

Tamwa inaendelea kuwatia shime waandishi wote kufanya kazi kwa bidii katika vyombo vyao vya habari na kuendelea kuwatia shime wanawake kushika ngazi za juu zaidi na pia wamiliki wa vyombo vya habari tunaendelea kuwahimiza waangalie waandishi wa habari wapewe kazi kulingana na uwezo wao.

Kwa mfano, wale waandishi ambao ni wanachama wetu, huwa wanahamasishwa kufanya kazi kwa bidii na tunao waandishi wanawake walio katika nafasi za juu na wanafanya vizuri.

Kwa hiyo, licha ya kwamba hatujafikia lengo, lakini ni kitu ambacho tunaendelea nacho katika kuwatia hamasa waandishi wa habari wanawake.

**SWALI:** Maeneo ya vijijini kuna waathirika wengi wa ukatili wa kijinsia. Tamwa ya Rose ina mkakati gani kuwasaidia wanawake wa vijijini kukabiliana na changamoto hii?

**REUBEN:** Ni kweli maeneo ya vijijini yana waathirika wengi wa ukatili wa kijinsia na Tamwa ilianzisha mabaraza saba nchini, na tumezifufua kamati za kupinga ukatili wa unyanyasaji wa jinsia, maarufu GBV Committee katika wilaya saba Tanzania Bara ambazo ni Kisarawe, Mvomero, Ruangwa, Lindi, Newala, Kitunda na Makumbusho na tatu zingine ziko visiwani Zanzibar.

Kamati hizi zinafanya kazi kubwa ya kuibua madhara ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto katika maeneo yao.

Lakini pia mkakati wetu ni kuendeleza yale mabaraza kuendelea kushirikiana na serikali za vitongoji, tunatamani kungekuwa na mabaraza kila wilaya au kata ili kuhamasisha, kufunza na kuwaelimisha watu kuwa ukatili wa kijinsia si kitu cha mtu mmoja, bali cha Watanzania wote.

Mkakati wetu ni kuangalia namna gani tunaweza kusogea mbele, haya saba yasiishie pale yalipoishia, tuongeze mengine kulingana na namna tunavyoweza k upata fedha.




## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza mbele ya Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (aliyekaa), ambaye alikuwa mgeni rasmi katika sherehe ya kukabidhi madarasa mawili yaliyojengwa na benki hiyo katika Shule ya Msingi Usa River wilayani Arumeru mkoani Arusha mwishoni mwa wiki, pia kuchangia madawati 40 vyote vikiwa na thamani ya shilingi milioni 60. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Ally Laay na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM aagiza uwezeshaji watafiti wa michikichi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Kilimo iwawezeshe watafiti katika kituo cha utafiti cha zao la michikichi cha Kihinga mkoani Kigoma, ili waongeze kasi ya uzalishaji wa mbegu bora za zao hilo.

Alisema serikali imeamua kuongeza nguvu kwenye michikichi, hivyo Wizara ya Kilimo hainabudi kukiwezesha kituo hicho kwa lengo la kuzalisha mbegu bora zitakazosambazwa kwa wakulima.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana alipotembelea kituo cha Kihinga kwa ajili ya kukagua shughuli za uzalishaji wa mbegu za michikichi, akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani Kigoma.

Alisema serikali imeamua kulifufua zao hilo kwa lengo la kumaliza tatizo la upatikanaji wa mafuta ya kula nchini, ambapo kwa mwaka inatumia zaidi ya Sh. bilioni 600 kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

"Wizara ya Kilimo iwawezeshe watu wa utafiti ili waendelee na shughuli hiyo kwa kasi, iwaongeze watumishi kituoni hapa na ongezeni nguvu kwenye zao la michikichi kama yalivyofanya mataifa mengine ya Costa Rica na Malaysia."

Alisema wakulima wa zao hilo wanahitaji kupata mafanikio, hivyo kituo hakinabudi kuongeza nguvu ya uzalishaji wa mbegu bora, ili wafikie malengo aliwashauri washirikiane na taasisi binafsi zinazozalisha mbegu.

Pia, Waziri Mkuu alisema Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Kihinga, kiendelee kutoa elimu na Wizara ya Kilimo ijenge majengo yake inayoyohitaji kwa ajili ya kufanyia shughuli za utafiti.

Mratibu wa Utafiti wa Kilimo kwa mikoa ya Tabora na Kigoma, Dk. Filson Kagimbo, alisema michikichi iliyopo sasa ina uwezo wa kuzalisha tani 1.6 ya mawese kwa hekta moja ambao kidogo na hauna tija.

Alisema mbegu wanazozizalisha zinalenga kumuongeza tija mkulima kwa kuwa zitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani nne kwa hekta, pia wanaendelea kuangalia vinasaba vya mbegu vilivyopo ili wazalishe mbegu bora zaidi.

"Tutakusanya vinasaba vyote vya mbegu tulivyonavyo na kuvitathmini na kuona uwezo wake na ikibidi tutaagiza kutoka nje ya nchi ili kuboresha zaidi." Miche ya michikichi inachukua muda wa miezi 18 kutoka hatua ya uchavushaji hadi kusambazwa kwa wakulima.

Baada ya kumaliza shughuli ya ukaguaji wa uzalishaji wa mbegu kituoni hapo, Majaliwa alikagua shamba la michikichi la Gereza la Kwitanga lenye ukubwa wa ekari 400 na kupanda mche kama ishara ya uzinduzi wa upandaji wa miche bora shambani hapo.

Waziri Mkuu amesema Serikali imeamua kuongeza nguvu katika zao hilo na inategemea taasisi zake mbili za Jeshi la Magereza (Kwitanga) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT-Bulombora), ambazo zina mashamba makubwa ya michikichi.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliagiza elimu kuhusu kilimo cha michikichi kuanzia hatua za awali hadi uzalishaji wa mafuta itolewe mashuleni ili wanafunzi waanze kupata ulewa na ifikishwe hadi kwa wananchi.

# Tanzania, Uingereza kuhifadhi misitu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), imeingia makubaliano na Shirika la Redcop linaloshughulika na Biashara ya Hewa Ukaa Duniani la Uingereza ambalo linashirikiana na kampuni inayojishughulisha na utafiti wa hewa ukaa (Livingway URT Ltd) la Tanzania kutekeleza mradi wa kuhifadhi misitu nchini.

Mradi huo utakaotekelezwa Mkoa wa Tabora kwa miaka 20 hadi 30, ambapo jumla ya Sh. bilioni 90 (paundi milioni 38 za Uingereza) zinatarajiwa kutumika ambazo zitatokana na vyanzo mbalimbali ikiwamo kutoka mashirika ya kimataifa yanayopambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mtendaji Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema hayo wakati wa hafla ya utiliaji wa saini kati ya serikali kupitia wakala huo na shirika hilo nchini iliyofanyika jana.

Prof. Silayo alisema programu ya uhifadhi wa misitu katika mkoa wa Tabora ni mojawapo ya programu zinazolenga kuchangia kwenye jitihada za dunia na serikali katika kupunguza vyanzo vinavyosababisha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema pia mradi umelenga kukabiliana na athari zake pamoja na kuchangia

INAENDELEA UK. 8

# Kamera za usalama zasimikwa Mirerani

**Na Mwandishi wetu**

AWAMU ya pili ya uwekaji wa kamera za kisasa (CCTV) katika ukuta wa machimbo ya madini ya tanzanite Mirerani mkoani Manyara imekamilika.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliyasema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa kituo cha mawakala wa kuuza Tanzanite.

"Ni muhimu sana kuzungusha ukuta kwenye eneo lenye madini yetu, lakini zaidi ni kuhakikisha eneo linalindwa muda wote katika kuhakikisha ulinzi na usalama kwa wafanyabiashara wa madini, mawakala na kodi za serikali zinakusanywa," alisema.

Kamera hizo, vifaa vya usalama na mashine mbalimbali zimesimikwa na Kampuni ya Starfix Enterprises kupitia Mhandisi Juma Kyando, ambaye alihakikisha vifaa hivyo vinaanza kufanyakazi ndani ya mwezi mmoja.

Waziri huyo alisema serikali ina mpango wa ujenzi wa kituo kimoja cha uuzaji na usafirishaji wa madini ya tanzanite, kitakachojengwa karibu na lango la kuingilia.

Kituo hicho kitakuwa na ofisi zinazotoa huduma mbalimbali kama vile huduma za benki, uhamiaji, huduma za ulinzi na usalama, ofisi ya kutoa vibali vya kusafirisha madini nje na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Mwishoni mwa mwaka jana, wataalamu kutoka ofisi ya Kamishna wa Madini, wakiongozwa na Kamishana wa Madini, Prof. Idris Kikula, walibaini kuna njia mbalimbali za utoroshaji madini na vito.

Aliyekuwa mwenyekiti wa timu hiyo, Prof. Kikula, alisema kuna baadhi ya mawakala wa madini walishiriki kutorosha madini kwa kupitia geti lililopo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dastan Kitandula, alisema Bunge limepitisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye madini na vito na kwamba kwa sasa kila mfanyabiashara atakuwa anawajibika kulipa kodi kwa serikali.


CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)
TUICO Street, Ilala Sharif Shamba P.O. Box 5680, Dar es salaam
E-mail: info@tuico.or.tz, Website: http://www.tuico.or.tz
Tel: +255 (0) 222 866 910 / 960, Fax: +255 (0) 222 866 911

**MAGARI/PIKIPIKI ZINAUZWA**
**(MOTOR VEHICLES AND MOTOR CYCLES FOR SALE)**

Maombi ya Zabuni yanakaribishwa kutoka kwa Wanachama, Wafanyakazi wote, Watumishi wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) na watu wengine kununua magari na pikipiki zilizoorodheshwa hapa chini. Magari yote yapo Ofisi ya TUICO Makao Makuu Ilala Shariff Shamba na pikipiki ziko Ofisi za TUICO mikoa ya Lindi, Rukwa , Shinyanga na Singida.

Magari na Pikipiki zimelipiwa kodi wakati wa kununuliwa. Mnunuzi atatakiwa kugharamia taratibu za kumilikisha (Ownership Transfer Formalities).

Magari na Pikipiki zitaangaliwa kwa kutembelea Ofisi ya TUICO Makao Makuu Ilala Shariff Shamba na Ofisi za TUICO Mikoa ya Lindi, Rukwa, Singida, Shinyanga na Singida muda wa kawaida wa saa za kazi.

Zabuni zote ziwasilishwe zikiwa zimefungwa vizuri kwenye bahasha zikiwa zimeandikwa **"ZABUNI YA KUNUNUA GARI/PIKIPIKI "**Zabuni zote ziwasilishwe Ofisi ya Katibu Mkuu TUICO na baada ya kuwasilisha Mzabuni ajiandikishe kwenye kitabu ambacho kitakuwepo kwa ajili hiyo.

Magari na Pikipiki ni haya yafuatayo, aina na hali ya gari:-

| NA. | NAMBA YA USAJILI | AINA YA GARI/PIKIPIKI | HALI YAKE | GARI/PIKIPIKI ILIKO |
|---|---|---|---|---|
| • | T 316 ADN | Toyota Land Cruiser | Inatembea | Makao Makuu |
| • | T 549 BSU | Toyota Land Cruiser | Inatembea | Makao Makuu |
| • | MC 165 AFE | Toyo | Inatembea | Lindi |
| • | MC 911 ADK | Honda | Haitembei | Shinyanga |
| • | T 860 ADK | Honda | Haitembei | Singida |
| • | T 872 ADK | Honda | Inatembea | Rukwa |

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 05/03/2019 saa 9.00 alasiri.

Maombi yatumwe kwa:-
**Katibu Mkuu,**
**TUICO Makao Makuu,**
**S.L.P. 5680,**
**DAR ES SALAAM.**

215064002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BUSARA

**VIJIKO SI LESENI YA KUTONAWA MIKONO**
**MIONGONI MWA MAELEKEZO YANAYOTOLEWA NA MABWANA AFYA NI PAMOJA NA KUNAWA MIKONO KABLA YA KULA. HATA UKITUMIA UMA NA VIJIKO BADO UTATAKIWA KUNAWA MIKONO YAKO. TUSISAHAU USAFI NI TABIA TENA KINGA DHIDI YA MARADHI. TUSICHOKE KUKUMBUSHANA.** NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI

# *Simba sasa fikirieni Caf, Yanga msitafute mchawi*

**BAADA** ya tambo nyingi kila upande ukijitapa kuibuka na ushindi, hatimaye mechi iliyosubiriwa kwa hamu kubwa ya watani wa jadi, Simba na Yanga, imepigwa Jumamosi na matokeo ndiyo kama mlivyosikia.

Mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa na Simba kushinda bao 1-0, Yanga ndiyo ilikuwa mwenyeji.

Na Simba ilipata ushindi huo ikitoka kuichapa Al Ahly kwa bao 1-0 kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Yanga ilitoka kupata ushindi kama huo Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania.

Hata hivyo, licha ya Yanga kupoteza bado inaendelea kuongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 58 baada ya mechi 24, wakati Simba iliyoshuka dimbani mara 16 yenyewe ikiwa na alama 39.

Nipashe tunafahamu mara baada ya mechi inayowakutanisha watani hao wa jadi, chokochoko nyingi hujitokeza katika klabu hizi mbili kutokana na presha kubwa kutoka kwa mashabiki ama wanachama.

Hiyo hutokana na kutoridhishwa na matokeo, hivyo ni nadra sana kumwacha mtu salama kwani pindi viongozi wanapopata presha kubwa hutafuta pakuponea.

Na katika harakati za kujinusuru, mara nyingi kama si baadhi ya wachezaji kufungiwa ama kutimuliwa kwa kutuhuma za kuihujumu timu kwa kucheza chini ya kiwango, basi huondoka na kocha.

Kawaida soka linamatokeo ya aina tatu, kushinda, kushindwa ama kutoka sare, hivyo mashabiki wanapaswa kukubaliana na kilichotokea na kuganga mbele kutazama mechi zijazo.

Ikumbukwe pia Yanga ipo kileleni mwa ligi hiyo ambayo bingwa huiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Lakini pia inakabiliwa na michuano ya Kombe la Shirikisho (FA Cup), ambayo bingwa hutoa tiketi ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Africa, hivyo chokochoko zozote za kuanza kutafuta mchawi zinaweza kuwaharibia kabisa na kukosa nafasi ya kucheza mashindano ya kimataifa baadaye mwaka huu.

Kadhalika, kwa upande wa Simba inabidi kusahau matokeo hayo na kuelekeza macho yake katika kucheza viporo vyake na mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba baada ya mechi hiyo, Simba inakabiliwa na mechi nne za Ligi Kuu mfululizo nyumbani na ugenini kabla ya kuifuata JS Saoura ya Algeria kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa.

Kwa mujibu wa ratiba, Jumanne Februari 19 itavaana na African Lyon kwenye Uwanja wa Shekh Amri Abeid jijini Arusha na kisha Februari 22, itakuwa Uwanja wa Taifa kukipiga na Azam FC kabla ya kuifuata Lipuli ya Iringa siku nne baadaye.

Machi 3, mwaka huu itaifuata Stand United ya Shinyanga na baada ya hapo itarejea jijini Dar es Salaam kujiandaa kuifuata JS Saoura ya Algeria tayari kwa kuvaana Machi 9 katika kinyang'anyiro hicho cha Mbingwa kinachoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

Ni wazi Simba ina ratiba ngumu, hivyo haina budi kupambana na huku ikijua ina jukumu zito la kuipeperusha vema bendera ya Taifa kimataifa, lakini pia ikikabiliwa na mtihani mzito wa kutetea ubingwa wake wa Ligi Kuu Bara.

Hivyo, ni wakati kwa timu zote mbili Simba na Yanga kusahau matokeo yaliyopita na badala yake kuelekeza akili kwenye mechi zijazo.

Aidha, mashabiki na wanachama wa klabu hizo hawana budi kukubaliana na matokeo kwani huo ndio utamaduni wa soka ambao ni kushinda, kushindwa ama kutoka sare.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Ucheleweshwaji adhabu TFF unapeperusha haki*

Na Adam Fungamwango

**WANASHERIA** wana msemo wao unaosema kuwa 'haki si tu itendeke, bali pia ionekane imetendeka.'

Ukiusoma kijuujuu unaonekana kama hauna maana sana na badala yake ni mbwembwe tu za wanasheria, lakini ukitulia utaelewa wana maana gani.

Na hata mtu anayepata adhabu ni lazima imuathiri, imuume ili siku nyingine asifanye tena.

Adhabu maana yake si kumkomoa mtu. Ni kwamba amefanya makosa ambayo anatakiwa apate uchungu ili ajutie na siku nyingine asirudie tena.

Kwa siku za karibuni naona kama Kamati za Shirikisho za Soka nchini (TFF), zilizowekwa kufanya kazi zake za kuadhibu wachezaji au kudhibiti wasifanye mambo yasiyo ya kistaarabu uwanjani, hazifanyi kazi zake vizuri.

Zinaonekana kujichanganya, kwa kuchelewa kutoa maamuzi, huku wengine maamuzi yao yakiwa ya papo kwa papo.

Kuna baadhi ya wachezaji wanapofanya makosa, basi haraka Kamati ya Saa 72 inafanya kazi yake bila kuchelewa, pamoja na Kamati yake ya Nidhamu, lakini kuna baadhi ya wachezaji wanapofanya makosa inashikwa na kigugumizi.

Nakumbuka misimu miwili iliyopita Kamati ya Saa 72 ilimsimamisha beki Abdi Banda wa Simba kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar siku moja tu baada ya mechi kumalizika.

Si hao tu, kuna baadhi ya wachezaji wengi ambao walikubwa na rungu la kusimamishwa muda mfupi baada ya kufanya makosa.

Hao ni Kelvin Yondani wa Yanga kwa kosa la kumtemea mate Asante Kwasi kwenye mechi ya watani wa jadi iliyochezwa Aprili 29, mwaka jana katika Uwanja wa Taifa ya msimu wa mwaka 2017/18.

Wengine ni James Kotei alipelekwa Kamati ya Saa 72 kwa kosa la kumpiga ngumi mchezaji wa Yanga, Gadiel Gabriel dakika ya 32 tukio ambalo mwamuzi hakuliona, pia Andrew Vincent wa Yanga alimpiga kichwa Mohamed Hussen 'Tshabalala' wa Simba na adhabu zao ilikuwa ni kufungiwa mechi tatu na faini ya milioni moja kwa kila mchezaji. Hata Erasto Nyoni na Hassan Dilunga imeshawahi kuwatokea. Hao ni baadhi tu.

Lakini inapokuja suala la mchezaji mwingine anafanya kosa, hasimamishwi bali anaendelea kucheza, tena hadi mechi mbili ndiyo anapelekwa, halafu inaonekana inaahirishwa-ahirishwa, haitendi haki.

Inaonekana kana kwamba hawa wachezaji wana matabaka. Kuna wachezaji wanagushwa na wengine hawagusiwi, bali wananyenyekewa.

Beki wa Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja' alimpiga kiwiko mchezaji Ayoub Lyanga kwenye mechi dhidi ya Coastal Union na tukio hilo kutoonwa na mwamuzi, yeye hajasimamishwa na amecheza mechi nyingine dhidi ya Singida United, pia dhidi ya Simba.

Inawezekana akaadhibiwa baada ya mechi hizo. Hapo ndipo ninapojiuliza inakuwaje wachezaji wengine wasimamishwe baada ya tukio na wengine waendelee hadi kucheza mechi mbili? Hii si halali na wala 'fair play' ambayo Fifa wanataka.

Fifa waliweka adhabu hizi ili wachezaji wajutie na wasirudie tena makosa. Adhabu inatakiwa impe uchungu mchezaji na iiathiri klabu yake ili watafute namna ya kukaa na kufundisha nidhamu mchezoni ili kutorudia makosa wanayoyafanya.

Sasa kama Ninja alifanya kosa na akaendelea kucheza mechi zilizofuata, hakuna umuhimu wowote wa kumfungia ila kumuacha tu.

Duniani kote mchezaji anapofanya makosa na kuadhibiwa, anatakiwa kutocheza mechi zinazofuata na si kuachwa acheze mechi moja, mbili au tatu, ndiyo afungiwe, labda awe anachunguzwa na vyombo husika.

Sasa inakuwaje Kamati za Kibongo ziwe zinawafungia 'fasta' tu wanapofanya makosa, na wengine kuwaacha kwanza wacheze baadhi ya mechi wakati kanuni ni zile zile na ligi ni ile ile? TFF na kamati zake ilitafakari hilo.

## BARUA/MJADALA

## *Tabia ya kuweka mambo ya kibinafsi hadharani inakera*

**Mhariri**

*Habari za majukumu!*

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

**Jackton Mwambungu**
**Mbagala.**

### WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Kwa hili, Siame wa Mbao FC anastahili tuzo




**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi binadamu huwa na tabia ya kueneza mabaya ya mwenzake kuliko mazuri yake.

Mwanadamu kama alivyo kiasili huwa na mazuri na mabaya, lakini mabaya huwa yanakuzwa zaidi na kuenezwa hata kama ni machache, kuliko mazuri aliyoyafanya.

Kuna mchezaji wa Mbao FC, Rafael Siame, amefanya jambo la kishujaa ambalo kwa sababu ni jema, si wengi wanaofahamu.

Ni kwa sababu jema, lakini kama lingekuwa baya uwanjani, lingekuzwa kwenye mitandao ya kijamii mpaka angepata adhabu kutoka ngazi za juu.

Mchezaji huyu ameokoa maisha ya mchezaji mwenzake Adeyum Saleh aliyekuwa katika hatari ya kupoteza maisha kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Mbao FC na Coastal Union iliyokuwa ikipigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kwenye mechi hiyo, wachezaji hao walikuwa wanacheza timu tofauti. Siame ni mchezaji wa Mbao iliyofungwa bao 1-0 dhidi ya Coastal ambayo alikuwa akichezea Adeyum.

Adeyum alianguka ghafla bila kuguswa na mtu yeyote, huku akiwa tayari aking'ata ulimi kitu ambacho ni hatari.

Siame, mchezaji wa timu pinzani ambaye alikuwa karibu yake, alikimbia na kuinama, akapitisha mkono kwenye kinywa cha Adeyum na kuutoa ulimi, hivyo kuokoa maisha yake, kabla ya watu wa huduma ya kwanza kufika sekunde chache baadaye.

"Sijui ni nini. Mechi za saa nane mchana nimeshacheza mara nyingi na bado naendelea kucheza, lakini leo sijui nini kimetokea. Nilihisi miguu imekosa nguvu nikaanguka, lakini namshukuru mchezaji mwenzangu wa Mbao kwa kuniokoa," Anasema Adeyum.

Daktari wa Coastal Union, Kitambi Mganga ameeleza sababu ni kupoteza maji mengi mwilini.

"Tatizo ni upungufu wa maji kwa sababu wachezaji wanapoteza maji mengi kwa kuvuja jasho na hii wakati mwingine husababishwa na kucheza wakati wa jua kali," anasema daktari huyo.

Kwa upande wa Siame, alisema kuwa wakati mwenzake akianguka na kupoteza fahamu aliimuona, hivyo alimkimbilia na kuingiza mkono kwenye kinywa cha Adeyum na kumsaidia baada ya kuona anang'ata ulimi.

"Huyu ni ndugu yangu japo ni timu tofauti, lakini tunaangalia utu zaidi. Nilikuwa wa kwanza kufika kwa sababu niliona anang'ata ulimi nikaweka mkono wangu kwenye kinywa chake ili kumsaidia. Sijawahi kupitia mafunzo yoyote ya huduma ya kwanza, lakini nilijikuta nikimsaidia kwa sababu nilikuwa wa kwanza kufika kwenye eneo la tukio."

Hili ni tukio ambalo haliwezi kupita bila kupongezwa na kuwa mfano kwa wachezaji wote nchini Tanzania. Tunaona mara nyingi uwanjani wakicheza wakipigana viwiko, kutemeana mate na kila aina ya ubabe, lakini hata mwenzao anapoanguka hawaendi hata kumtazama na badala yake kuwakimbilia waamuzi kujitetea kuwa hawajafanya kitu.

Wengine hata wachezaji wa timu pinzani wanapoanguka wanawakanyaga kabisa.

Siame ametuonyesha kuwa mpira si uadui. Ni upinzani tu wa ndani ya dakika 90 na hata ndani ya dakika hizo kuna matukio wachezaji wanaweza kusaidiana.

Bado sijasikia kauli yoyote kutoka kwa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), wala Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo (TASWA) na hata Chama Cha Wachezaji nchini (SUPTANZA) juu ya angalau kupongeza ya kilichofanywa na mchezaji huyu shujaa. Labda watafanya hivyo baadaye.

Ninachokitaka hapa ni kwamba tusiwe na tabia ya kujitokeza kukanya, kuadhibu wakati wachezaji hawa wanapofanya makosa tu, lakini hata wanapofanya vitu vizuri kama hivi inabidi tutoe angalau pongezi. Hii itawafanya hata wachezaji wengine kujifunza na kutaka kuiga mfano wake.

Hatutakiwi kuwa vipofu hadi pale mtu anapofanya mabaya, Siame anastahili zawadi kama si tuzo ya kutukuka ya mchezaji bora wa mwaka wa 'Fair Play' na pia hata 'asante' kidogo kwa alichokifanya ambacho ni aghalabu sana kufanywa na wachezaji hasa wa Kiafrika, achilia mbali wanaocheza soka Bongo.

## KABWELA

**NA FADHIL MOHAMMED**



# Gereza kupatiwa kiwanda cha kisasa kukamulia mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara ihakikishe gereza la Kwitanga mkoani Kigoma linapata kiwanda bora na cha kisasa cha kukamulia mafuta ya mawese kitakachoonesha dhamira ya Serikali ya kufufua zao la michikichi nchini.

Hata hivyo, Waziri Mkuu amesema ameridhishwa na jitihada zilizofanywa na Jeshi la Magereza katika kuboresha shamba lake la michikichi pamoja na mabadiliko waliyoyafanya kwenye kiwanda chao cha kuzalisha mafuta.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipotembelea Gereza la Kwitanga kwa ajili ya kukagua shamba la michikichi na kuzindua trekta na kufungua sero moja iliyojengwa gerezani hapo.

Alisema amefurahishwa baada ya kukuta mashine mpya ya kukamulia mafuta ya mawese inafungwa kwenye kiwanda cha gereza hilo ambayo itakuwa inatumia mota tofauti za zamani wapolikuwa wanatumia mashine ya kusukumwa na mikono.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliliagiza Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) waimarishe teknolojia ya kukamua mafuta kwenye kiwanda hicho ili kiweze kuzalisha kwa tija.

Katika kuhakikisha gereza hilo linakuwa la mfano kwenye kilimo cha zao la michikichi, Waziri Mkuu aliiagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inunue gari lenye winchi litakalorahisisha uvunaji wa chikichi.

Amesema njia inayotumiwa kwa sasa ya kupanda juu ya mchikichi wakati wa mavuno si salama kwa mvunaji, hivyo ni vema wakatumia magari hayo yenye winchi kwa ajili ya kurahisisha shughuli ya uvunaji.

Kwa upande wake, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Kigoma, Leonard Burushi, alisema wamefanikiwa kuongeza uzalishaji wa mafuta kutoka pipa 63.4 kwa mwaka 2016/2017 na kufikia pipa 97 kwa mwaka 2018/2019 na zoezi la uvunaji linaendelea.

Alisema mafanikio hayo yametokana na maagizo yalitolewa na Waziri Mkuu alipotembelea gereza hilo Julai, 2018, ambapo pamoja na mambo mengine, aliwaagiza waboreshe eneo la kukamulia mafuta ili waongeze uzalishaji.

Alisema kuwa eneo la ekari 20 limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kukamua mafuta ya mawese, maghala ya kutunzia mafuta machafu na upanuzi wa kiwanda baadae.

Alieleza kwamba maelekezo mengine yaliyotolewa na Waziri Mkuu ni pamoja na Magereza ya Kwitanga na Ilagala yaongeze eneo la mashamba yake kwa ajili ya kupanda michikichi mipya ambalo limetekelezwa.

Kwa mujibu wa Burushi, gereza la Ilagala limeandaa jumla ya ekari 150 zenye uwezo wa kupandwa michikichi aina ya tanera 8,550 na Kwitanga ekari 400 ambazo zitapandwa miche 22,800 ya michikichi aina ya tanera.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (aliyeshika nyavu), akimwonyesha Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa (kulia kwake), tofauti ya nyavu zinazotakiwa kutumiwa katika shughuli ya uvuvi zilizokamatwa katika eneo la Mlingotini wakati wa ziara yake ya siku moja katika wilaya hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## Tanzania, Uingereza kuhifadhi misitu

INATOKA UK. 5

maendeleo endelevu kwa wananchi wa mkoa huo na mikoa jirani pamoja na taifa kwa ujumla.

Mtendaji huyo mkuu alisema programu hiyo inalenga kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kufanikisha fursa, changamoto na namna ya kufanikisha uhifadhi endelevu na maendeleo ya wananchi.

"Lengo kuu la programu ni kuongeza thamani ya maliasili zilizopo na kuchangia katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na maendeleo endelevu," alisema Prof. Silayo.

Alisema kwa kuanzia programu itatekelezwa katika misitu ya hifadhi zenye ukubwa unaokadiriwa kufikia hekta milioni 3.6 na matokeo chanya ya mradi huo yatajumuisha kuimarisha uhifadhi wa misitu kwa kutatua changamoto ya shughuli zote zinazochochea uharibifu wa misitu kwa kuibua fursa mbadala za kuwapatia wananchi kipato.

Prof. Silayo alisema wananchi watawezeshwa kufanya shughuli ambazo ni rafiki wa uhifadhi wa misitu na mazingira kwa ujumla na katika kutekeleza mradi huo utawezesha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya nyuki, mazao ya kilimo na mifugo, pamoja na kuimarisha miundombinu ya huduma za jamii na maendeleo kwa wananchi.

"Makubaliano haya ni mwanzo mzuri wa kupunguza uharibifu wa misitu, kuongeza kipato cha jamii na kupunguza athari zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi nchini," alisema Prof. Silayo.

Naye Mkurugenzi wa Masoko na Uendeshaji kutoka Reddcop Uk, Askofu Dk. Ernest Irung, alisema mchakato wa kuanzishwa mradi huo ulianza Aprili 13, 2013 na kujulishwa serikali na mwaka 2014, mchakato uliharakishwa ikiwamo kufanyia utafiti maeneo mbalimbali ya mkoa wa Tabora, ambapo michakato yote ilikamilishwa mwaka 2015.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Livingway URT Tanzania, Eston Kasika, aliishukuru serikali, TFS na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuona wananchi wananufaika na rasilimali za maliasili za taifa.

Alisema kwa pamoja watashirikiana bega kwa bega na TFS, ili kufanikisha mradi huo kwa manufaa ya wananchi na taifa na kwamba eneo lililotolewa kufanyiwa kazi kwa kuwa ni sawa na keki ya taifa. Mratibu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Hewa Ukaa (NCMC) kilichopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Eliakimu Zahabu, alisema kituo hicho kilianzishwa kwa ajili ya kutengeneza takwimu za msingi ambazo watu na vikundi mbalimbali viweze kufikia na kushiriki kwenye biashara ya hewa ukaa nchini.

## Samia aipa tano TADB

INATOKA UK. 3

vyetu," alisema.

Mwakilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo ambaye ni Mkurugenzi wa Mikopo na Biashara, Augustino Matutu Chacha, alisema kwa msimu huu wa mwaka 2018/2019, benki imeidhinisha mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3.506 kwa miradi ya kilimo ya Mkoa wa Singida pekee, ambapo shilingi bilioni 1.285zimetolewa kwa ajili ya miradi ya kilimo cha alizeti kwa wakulima 458 walio chini ya AMCOS na shilingi bilioni 2.221 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kusindika mbegu za mafuta ya alizeti kitakachojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

"Tunatambua alizeti kama mojawapo ya mazao ya kimkakati kwa uchumi wa taifa letu na hasa kwa wananchi wa mikoa inayozalisha zao hili kwa wingi ikiwamo mkoa wa Singida. Zao hili la Alizeti lina fursa kubwa ya kuliingizia taifa fedha za kigeni na pia ni chanzo cha ajira kwa watu wapatao laki 3 na zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa mkakati wa benki hiyo ni kuendelea kusaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa alizeti zenye ubora kwa ajili ya kusaidia viwanda vya ndani kupata malighafi.

Kwa mujibu wa Chacha, benki imefanya mazungumzo na inatarajia kukutana na wadau wasindikaji wa mafuta ya kula kwa lengo la kuandaa mpango shirikishi wa kutoa huduma za pembejeo na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima.

Mmoja wa wanufaika wa mkopo huo, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika, Yahya Ramadhan, alisema ujio wa Benki hiyo umerudisha ari ya wakulima wa alizeti mkoani Singida ambao kwa takribani miaka nane wameshindwa kulima kwa tija kutokana na ukosefu wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo.

# Maelfu ya wazee kupata bima afya

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imetenga kiasi cha Shilingi milioni 11.7 kwa ajili ya kuwakatia wazee 2,340 kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF), ili kuwaboreshea huduma bure za matibabu.

Halmashauri hiyo ina jumla ya wazee 10,232 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, ambapo mpaka sasa waliokatiwa bima hiyo ni 6,247 na kusalia 3,985.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Ustawi wa Jamii wa halmashauri hiyo, Abrahmani Nuru, wakati akisoma taarifa kwa niaba ya Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Lukas Ngamtwa, kwenye kikao cha shirika la kutetea haki za wazee mkoani Shinyanga, (Tawlae), kuhusiana na namna serikali inavyotatua changamoto za wazee. Alisema katika mwaka wa fedha 2018-19, walitenga Shilingi milioni 10 na kukatia wazee 6,247 bima hiyo na kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2019-20, wametenga Shilingi milioni kuwakatia wazee 2,340 bima hiyo kwa kila kichwa Shilingi 30,000.

"Utengaji wa bajeti hizi za fedha za wazee kwenye halmashauri yetu itakuwa endelevu ili kutatua changamoto zao za matibabu, ambapo pia tumeweka mkakati wa kila baada ya miezi sita tunabaini wazee wapya ambao wameshafikisha umri wa miaka 60 ili kuwakatia CHF," alisema Nuru.

"Mbali na ukataji wa CHF, pia fedha hizi ambazo huzitenga hutumika katika matumizi mbalimbali yakiwamo maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani pamoja na kuendeshea vikao vyao, ili kuonyesha uthamani wa wazee katika nchi yetu ambao ndio waliopigania uhuru wa taifa hili," aliongeza.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la Halmashauri ya Kahama Mji, Wilfred Bilago, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kutenga bajeti ya fedha ya kuwakatia CHF, kwa kuwa idadi yao kubwa hawana uwezo wa kifedha wa kupata matibabu kutokana na kukosa nguvu ya kufanya kazi na wengine wakitelekezwa na watoto wao.

# Wahisani Korea wasaidia walioathiriwa na floride

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI ya Korea Kusini imetoa Dola za Kimarekani 40,000 kununua mtambo wa kuondoa madini ya floride kwenye maji katika Kijiji cha Landalai, Kata ya Oldonyo Sambu, wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Mtambo huo utasaidia kuondoa tatizo la floride, chumvi na bakteria wenye madhara kwenye maji katika eneo hilo ambalo wananchi wengi wameathiriwa na tatizo la kupinda miguu kutokana na kutumia maji yenye madini hayo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo wa wahisani kutoka Korea Kusini, Mwakilishi wa Kampuni ya O2&B, Seughyun Bahn, aliyekutana na wataalamu na watafiti mbalimbali kutoka kanda za kaskazini na kati, alisema madhara ya madini ni makubwa kwa binadamu.

"Mchango wetu katika hili utasaidia kupunguza matatizo ambayo wananchi wa eneo hili wamekuwa wakiyapata," alisema na kuongeza kuwa kampuni yake imeguswa sana na tatizo ambalo wananchi wamekuwa wakiathirika.

Wataalamu waliokuwapo katika uzinduzi huo walisema katika maeneo mengi ya vijijini kumekuwapo na tatizo la floride na chumvi ambayo mara nyingi imekuwa ikibadilisha rangi ya meno na mifupa.

"Limekuwa ni tatizo kubwa linalosababisha wananchi washindwe kushiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo," alisema mmoja wa wataalamu hao,

Akizungumza baada ya kufunguliwa mradi huo, Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Arusha anayeshughulikia Sekta ya Maji kwa kushirikiana na watafiti wa ndani na nje, Mhandisi Emmanuel Makaidi, mbali ya kushukuru msaada huo, alisema mtambo huo utasaidia wananchi katika eneo hilo.

"Ujio wa teknolojia hii utasaidia sana kupunguza tatizo kama siyo kulitokomeza kabisa," alisema Mhandisi Makaidi.

Kwa upande wake, mdau wa maendeleo, Gaudence Kayombo, alisema hatua zilizochukuwa zitasaidia kutatua tatizo ambalo lilidumu kwa muda mrefu.

"Wakazi wa eneo hili wengi wao waliathirika na tatizo hili kwa kiasi kikubwa. Ni imani yangu sasa watajikita kwenye shughuli za maendeleo," alisema Kayombo ambaye pia ni Mbunge mstaafu wa Mbinga.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Oldonyo Sambu wameulezea mradi huo kuwa ni mkombozi mkubwa kwao na watoto.

Raymond Lerumbe, amabye ni mkazi wa Oldonyo Sambu na Mwalimu Role Ngalama hawakuweza kuficha furaha yao kwa mradi huo waliouelezea kuwa ni mkombozi kwa maisha yao na vizazi vijavyo.

"Tunaomba serikali kwa kushirikiana na wafadhili waendelee kutusaidia kupitia mradi huu ambao ni muhimu sana kwetu."



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Shilingi 11,270,000 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, kwa ajili ya kununulia mifuko 1,000 ya saruji kama mchango wa NBC kuchangia ujenzi wa kituo cha polisi cha Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi. Hafla ya makabidhiano iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: PMO**

# Waliokosa madarasa Mkuranga sasa kuanza masomo mwezi ujao

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, imeanza ujenzi wa miundombinu ya majengo ya madarasa na maabara ili kuwawezesha wanafunzi waliokosa nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza mwezi ujao.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mshamu Munde, katika kikao cha Baraza la Madiwani.

Kikao hicho cha mwishoni mwa wiki kilikuwa kinapitisha bajeti ya Shilingi bilioni 30 kwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Munde alisema kutokana na wanafunzi zaidi ya 1,000 kukosa nafasi za kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, wilaya imelifanyia kazi suala hilo.

Alisema shule tatu zilijengwa, lakini zilikosa vigezo vya kusajiliwa kutokana na kutokuwa na maabara.

Alizitaja shule zilizojengwa za sekondari ni Mwandege ambayo haikuwa na jengo la maabara, lakini sasa imetengwa Shilingi milioni 45 kwa ajili ya ujenzi.

Aliongeza kuwa shule nyingine ni Mlamleni na Miteze ambazo zimetengewa Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kujenga maabara na matundu ya vyoo.

Alisema mpaka Machi mwaka huu shule zote zitakuwa zimekamilika kwa ajili ya kuchukua wanafunzi waliokosa nafasi.

Munde alisema kuwa baadhi ya wanafunzi waliokosa nafasi walijiunga na masomo katika shule za binafsi na kwamba idadi ndogo ya wanafunzi iliyobaki itaingia katika shule hizo mwezi ujao.

# Wanafunzi watishiwa magonjwa hatari

**Na Daniel Limbe,** CHATO

WANAFUNZI wa shule za msingi wilayani Chato mkoani Geita, wapo hatarini kuugua magonjwa ya kuhara, kutapika, fangasi pamoja na magonjwa ya zinaa kutokana na kuchezea mipira ya kiume (condom).

Hatua hiyo inatokana na baadhi ya wakazi wa kata ya Chato kufanya mapenzi ndani ya vyumba vya madarasa ya Shule ya Msingi Kitela nyakati za usiku kisha kutelekeza mipira hiyo, ambayo baadaye huokotwa na wanafunzi na kutumia kwa kupuliza bila kutambua madhara wanayoweza kuyapata.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Paulo Samwel, aliliambia Nipashe kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikifanyika kutokana na kukosekana mlinzi kwenye shule hiyo.

"Ukweli inasikitisha sana kuona baadhi ya wazazi tena wakiwa na akili zao timamu wanaamua kufanya mapenzi ndani ya vyumba vya madarasa...

"Kibaya zaidi baada ya kumaliza vitendo hivyo hutupa mipira hiyo ndani ya darasa bila kujali wanafunzi hasa wa darasa la awali huokota na kuanza kupuliza, wakiamini ni vipulizo."

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kitela, Honest Alex, alithibitisha vitendo hivyo kufanyika katika vyumba vya madarasa hayo, na kwamba hali hiyo husababishwa na shule hiyo kukosa ulinzi pamoja na uzio.

Aliiomba serikali kuhakikisha inazisaidia shule za msingi kupata walinzi ili kunusuru afya za watoto pamoja na samani za shule.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Paulo Butondo, mbali na kukiri kutokuwa na mlinzi shuleni hapo, alisema mwaka jana wazazi walishindwa kuchangia fedha kwa ajili ya malipo ya mlinzi kutokana na kauli ya Rais John Magufuli ya "elimu bure na iwe bure kweli."

Alisema maelekezo hayo kwa kiwango kikubwa yaliwafanya wazazi wasiwe tayari kuchangia fedha kwa ajili ya mlinzi.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Chato, Rigobert Kalisa, alisema vitendo hivyo ni hatari kwa afya za watoto na kwamba kuna haja ya wazazi na serikali kushirikiana kuondoa changamoto hiyo.

Alidai kuwa mipira hiyo inapotumika kisha kutupwa hugeuka taka ambayo inaweza kuathiri afya za wanafunzi wanaozipuliza ikiwamo kuugua magonjwa ya kuhara, kutapika, fangasi na hata magonjwa ya zinaa iwapo waliotumia walikuwa na magonjwa hayo.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Charles Kichere (aliyeshika chupa), akikagua namba za kielektroniki kwenye bia hiyo, alipotembelea kiwanda cha TBL tawi la Mwanza kuona mashine ya stempu ya kielektroniki ikiweka namba kwenye kinywaji hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasomi kutumika kutangaza utalii

**Na Ashton Balaigwa,** IRINGA

HIFADHI ya Taifa ya Ruaha, imeanzisha programu maalumu ya kuwatumia wasomi kwa ajili ya kuwa mabalozi kutangaza vivutio vya utalii ili kuhamasisha Watanzania kuutembelea.

Chini ya mpango huo, hifadhi hiyo imeamua kuvishirikisha vyuo vya elimu ya juu 20 vilivyoko katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mbeya, Iringa na Dar es Salaam.

Akizungumzia mpango huo mbele ya viongozi wakuu wa serikali za wanafunzi wa vyuo hivyo, Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha Izumbe Msindai, alisema lengo lake ni kuongeza idadi ya wageni kutoka nchini ili waendane sambamba na wageni kutoka nje ya nchi.

"Tumeamua kushirikisha wanazuoni hawa ili wawe mabalozi wa kutangaza utalii wa ndani ambao kwa hapa kwetu umekuwa ukidorora kutokana na Watanzania kutotembelea hifadhi nchini," alisema.

Alisema kwa sasa hifadhi hiyo inatembelewa na wageni wapatao 25,000 kwa mwaka, lakini watalii wa ndani ni 8,000, na waliobaki 17,000 ni watalii wa kutoka ng'ambo.

Alisema makundi ya wasomi yatasaidia kueneza sifa za hifadhi hiyo ambayo ina vivutio vingi, ingawa haijatangazika sana.

Msindai alisema hifadhi hiyo ndiyo inayoongoza kwa ukubwa nchini na kwamba ina vivutio vingi ambavyo ni adimu katika hifadhi zingine.

"Hapa Ruaha zipo aina mbalimbali za wanyama na ndege ambazo zipo hatarini kutoweka duniani, aina hizi unazikuta katika hifadhi hii pekee," alisema.

Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Iringa, ambaye pia ni Mkuu wa Idara ya Utalii na Utamaduni chuoni hapo, James Sanga, alisema kwa kutumia wasomi hao kutaongeza hadhi ya hifadhi za kusini na kwamba itasaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza utalii huo.

Aziz Juma, Rais wa Serikali ya wanafunzi Chuo cha Mipango Dodoma, alisema kuna haja kuandaa mikakati kabambe ya kufikisha ujumbe kupitia klabu za wanafunzi kila chuo nchini.

# Magereza watekeleza agizo la JPM

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Magereza mkoani Rukwa, limefanikiwa kuongeza maeneo ya uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka hekari 700 hadi 1,400, lengo ni kupanua wigo wa kulisha wafungwa na mahabusu katika magereza yaliyoko katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Songwe na Mbeya.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Magereza mkoani Rukwa, Jail Mwamgunda, alipotembelea ofisi za magereza mkoani humo, ili kujua mikakati waliyojiwekea tangu Rais John Magufuli ambaye aliliagiza jeshi hilo lianze kujitegemea.

Mwamgunda alisema Gereza la Mollo lililoko nje kidogo ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga limeongeza eneo la kulima mahindi, ambapo kabla ya msimu wa kilimo huu lilikuwa likizalisha mahindi kwenye mashamba yenye ukubwa wa hekari 400, lakini sasa linazalisha katika ukubwa wa hekari 1,000.

Alisema katika msimu wa kilimo ulioanza Novemba mwaka jana, wamefanikiwa kulima hekari 805 za mahindi na wamepalilia, hivyo wanatarajia kuvuna magunia 9,660 sawa na wastani wa gunia 12 kwa hekari moja.

Kuhusu zao la maharage, Mwamgunda alisema yanalimwa kwa misimu miwili katika mwaka na kwamba wanatarajia kulima hekari 400 tofauti na miaka ya nyuma ambapo walikuwa wanalima hekari 100.

Alisema kuwa pamoja na mafanikio hayo, lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendea kazi kwa kuwa wana matrekta matano ambayo hayatoshi.

Hali hiyo pia inatokana na kutumia wanyama kazi pamoja na kilimo cha mkono.

Mkuu huyo wa magereza mkoa alisema kuwa iwapo wakifanikiwa kupata vitendea kazi, wataongeza uzalishaji na tija, kwa kuwa lengo ni kutekeleza agizo la Rais la kulitaka jeshi hilo kuhakikisha kuwa linaongeza uzalishaji.



Wadau wa madini ya tanzanite mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakiandamana kumuunga mkono Rais John Magufuli kwa kuwajali juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mmoja mbaroni, 3 wasakwa tuhuma mauaji ya mwenyekiti

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

POLISI mkoani Manyara, wanamshikilia mkulima na mkazi wa Kijiji cha Gijedabung, Limito Lebangu, (19), na kuendelea kuwasaka watuhumiwa watatu wa mauaji ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Gijedabung, Faustine Sanka, (59).

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, alisema wauaji walifanya hivyo wakidai mwenyekiti alikuwa akizuia na kuwaripoti kwa askari wa wanyamapori baadhi ya vijana wanaofanya shughuli za ujangili ndani ya hifadhi hiyo.

Baada ya mauaji hayo, yaliyotokea Februari 14 saa 11:00 jioni maeneo ya Gurusi ndani ya Hifadhi ya Taifa Tarangire, mwili wa marehemu ulitupwa katika hifadhi hiyo.

Taarifa za kuchinjwa kwa mwenyekiti huyo zilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Kamanda Senga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na matukio mbalimbali yaliyotokea mkoani humo.

Alisema tukio hilo lilitokea Februari 14 saa 11:00 jioni huko maeneo ya Gurusi ndani ya Hifadhi ya Taifa Tarangire katika kijiji hicho, ambapo alisema mwenyekiti huyo alikutwa amefariki dunia na mwili wake ukiwa umebaki miguu na viungo vingine vya mwili vikiwa vimeliwa na wanyama.

"Kabla ya tukio hilo marehemu aliondoka nyumbani kwake Februari 9, 2019 saa 12 jioni akiwa na pikipiki yenye namba za usajili T 942 BKE, rangi nyekundu, toka siku hiyo hakuonekana mpaka alipokutwa amefariki dunia, huku mwili wake ukiwa umetupwa ndani ya hifadhi," alisema.

Kamanda Senga alimtaja aliyekamatwa kwa tuhuma za mauaji hayo kuwa ni Limito Lebangu (19), mkulima na mkazi wa Gijedabung, ambaye amekamatwa na kukiri kuhusika na mauaji akiwa na wenzake watatu ambao aliwataja kuwa ni Miraji Hidikimu, Hamis Hussein na Aziz ambaye alifahamika kwa jina moja.

"Mbinu waliyotumia ni kumchinja shingo kwa kutumia kitu chenye ncha kali kisha kumweka kwenye mfuko wa sandarusi na kufunga katika pikipiki na kutupa ndani ya Hifadhi ya Taifa Tarangire, ambapo pikipiki ilipatikana eneo la tukio," alisema.

Aidha, alisema chanzo cha tukio hilo ni marehemu huyo kuzuia na kuwaripoti kwa askari wa wanyamapori baadhi ya vijana wanaofanya shughuli za ujangili ndani ya hifadhi hiyo.

Hata hivyo, upelelezi unaendelea kwa kuwasaka wengine ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria. Katika hatua nyingine polisi wanamshikilia, Ramla Omari, (23), mkulima na mkazi wa Nangara kwa tuhuma za kutupa kichanga alichojifungua, tukio hilo lilitokea Februari 12 saa 3:00 asubuhi, ambapo alitupa kichanga hicho katika shimo la kichuguu lililoko karibu na nyumbani kwao mara baada ya kujifungua.

"Kabla ya tukio hilo mtuhumiwa alihisi kuumwa na uchungu na ndipo aliamka na kuchukua ndoo iliyokuwa na maji kwa lengo la kutaka mtoto asitoe sauti mara baada ya kutoka tumboni, hivyo mtoto huyo alikosa hewa kisha kufariki ndipo mtoto huyo alichukuliwa na mama yake na kutupwa shimo la kichuguu," alifafanua.

Kamanda alisema mama huyo alipohojiwa kuhusu tukio hilo alisema chanzo ni ugumu wa maisha na mwili wa mtoto huyo umehifadhiwa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Mji wa Babati Mrara.

# Wajumbe wawakumbuka yatima kwa chakula

**Na Mwandishi Wetu,** MIRERANI

WAJUMBE wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani, wamejitolea magunia matatu ya mahindi, mchele kilo 100 na lita 10 za mafuta ya kupikia kwa kituo cha Light in Africa kinacholea watoto yatima na wenye kuishi katika mazingira magumu.

Mwenyekiti wa mamlaka hiyo, Adam Kobelo, alisema baada ya wajumbe na wataalamu wa mamlaka hiyo kujionea maisha ya watoto wa kituo hicho, waliona ni vema wakijitoa na kuchanga kidogo walichonacho ili kusaidia chakula.

Hata hivyo, Kobelo alisema mwishoni mwa wiki kuwa ingawa walichokitoa ni kidogo, yaani, vyakula vya thamani ya Sh. 400,000 tu, lakini wamejitolea kwa moyo mmoja.

Alisema kitendo cha kuwatunza watoto yatima na wenye kuishi katika mazingira magumu ni jambo kubwa kwa kuwa siyo watu wengi wanaoweza kufanya hivyo.

"Pia kwa kutambua mchango wako kwa jamii sisi kama mamlaka ya mji mdogo wa Mirerani tunakupatia cheti cha kutambua kazi unazozifanya na tutazidi kushirikiana zaidi ya hapa," alisema Kobelo.

Paroko wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria, Mama wa Rozari Takatifu, Padri Vincent ole Tendeu, alisema wanafunzi wanaosoma shule katika kituo hicho wanapaswa kupewa kipaumbele shuleni na kuepuka kutowanyanyapaa.

Padri Ole Tendeu alisema jamii inapaswa kuunga mkono kituo hicho kutokana na kujitoa kwa mama huyo.

Mwanzilishi wa kituo cha Light in Africa, Lynn Elliott, aliwashukuru wajumbe hao na kusema hana mdhamini zaidi ya Mungu.

Alisema awali alikuwa anahudumia watoto kwenye kituo chake kilichokuwa Bomang'ombe, wilayani Hai, lakini hivi sasa amehamia mji mdogo wa Mirerani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani, Evence Mbogo, alisema mama Lynn amekuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na jamii kwenye matukio mbalimbali.

Alisema mama Lynn ameshashiriki kuhamasisha jamii kusafisha mazingira ya mifereji ya barabara, makaburi na kujitolea damu kwa Kituo cha Afya Mirerani.

# Vijana CCM wahimizana kugombea

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JUMUIYA ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, (UVCCM), wilayani Arusha, imewataka vijana kujitokeza kwa kugombea nafasi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa baadaye mwaka huu.

Kadhalika jumuiya hiyo imewataka vijana wote wilayani hapa kuwa wazalendo, waaminifu na wawe waadilifu katika nafasi zao na shughuli wanazofanya, lengo likiwa ni kurejesha heshima ya jumuiya hiyo.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa UVCCM, Wilaya ya Arusha, Saipulani Abubakary Ramsey, wakati akizungumza na waandishi.

Alisema katika uongozi wake atajitahidi kuwainua vijana kiuchumi ikiwamo kuanzisha mradi mkubwa wa mazao ya mifugo na nafaka.

"Uongozi wangu nitafanya kwa vitendo katika kuunga mkono jitihada za Rais Dk. John Magufuli kutekeleza sera ya viwanda na uchumi wa kati," alisema.

Alisema viongozi waliopo pamoja na yeye watahakikisha wanasimamia rasilimali za chama na jumuiya hiyo.

"Niko tayari kutoa kiasi kidogo ninachokipata kusaidia mambo ya jumuiya ikiwamo walinzi wa viongozi na chama (green guard), nitatoa mavazi na vifaa kwa vijana wetu, kwa kuwa sisi vijana ndio nguzo ya chama chetu," alisema.

Aliongeza katika uongozi wake atashirikiana na wadau mbalimbali yakiwamo mashirika na taasisi, zikiwamo sekta binafsi kuanzisha mashamba ya mazao ya nafaka na mifugo, ambapo ajira itaongezeka kwa vijana.

Hata hivyo, Saipulani, aliongeza vijana wanatakiwa kuwa na nidhamu, uadilifu na uzalendo, huku akiwaonya baadhi ya vijana wanaozunguka na kuisemea jumuiya hiyo bila utaratibu waache kwa sababu katika uongozi wake jambo hilo litakomeshwa.





# Dk. Mengi atunukiwa tuzo hifadhi mazingira

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi, ametunukiwa tuzo ya mafanikio katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira hasa kutokana na mchango wake alioutoa mkoani Kilimanjaro kwa kupanda miti zaidi ya milioni 24.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amemwelezea Dk. Mengi kuwa ni miongoni mwa wadau muhimu kutoka sekta binafsi ambao wametoa mchango mkubwa katika sekta ya mazingira kwa ujumla wake.

Mghwira alikabidhi tuzo hiyo mwishoni mwa wiki, kwa Ofisa Utumishi wa Kampuni ya Bonite Bottlers Ltd, Joyce Mushi, kwa niaba ya Dk. Mengi, wakati wa kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa huo (RCC).

"Sisi kama serikali, tunatambua mchango mkubwa unaotolewa na Mwenyekiti wa Kampuni za IPP, Dk. Regnald Mengi, kwa kutunza mazingira, kupanda miti na kutoa vifaa mbalimbali vya kusaidia shughuli za mazingira.

"Hata hivyo bado tuna changamoto katika mkoa wetu wa Kilimanjaro ya suala la utunzaji wa mazingira, bado sio la kuridhisha," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Baada ya kupokea tuzo hiyo, Mushi aliishukuru serikali kwa kutambua mchango wa Dk. Mengi katika suala la utunzaji wa mazingira, akisema utunzaji na uhifadhi wa mazingira nchini ni sehemu ya maono aliyonayo Dk. Mengi.

Wengine waliotunukiwa tuzo hiyo ni Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TaCRI), ambao wamewezesha kupandwa miti na miche ya kahawa zaidi ya milioni 21, Kampuni ya Sukari TPC, asasi ya kiraia ya Floresta Tanzania na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa).

Awali, Ofisa Mazingira wa Mkoa wa Kilimanjaro, Sperancea Gabone, alisema tuzo hizo zilizotolewa ni kwa washindi wa mwaka jana.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na wabeba mizigo na waongoza watalii kuhusu maslahi madogo wanayolipwa na baadhi ya kampuni za watalii, ambayo ni kinyume cha sheria, alipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro katika geti la Mweka, kwa ajili ya kusikiliza kero hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibano chawadhibiti madalali upangishaji maeneo ya biashara

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MSIMAMO usioyumba wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, kuhusu bei elekezi ya soko la ukodishaji wa maduka ya biashara katika kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani, umewanyong'onyeza watu wanaodaiwa kucheza 'dili' la kukodi maeneo hayo na wao kukodisha kwa bei ya kuruka kwa wafanyabiashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa hiyo, Michael Mwandezi, amesema wanaolalamika kuhusu bei elekezi ya sasa ya Sh. 450, 000 kwa maduka ya chini na Sh.400, 000 kwa maduka yaliyoko ghorofa ya kwanza ni wachuuzi, wao hawafanyi biashara.

"Baada ya kujitokeza kelele kelele, ilibidi tuchunguze zaidi, hizi kelele zinatoka wapi, tukagundua ni watu ambao ni wachuuzi, sio wao wanaofanya biashara. Kwamba wao wanachukua vibanda wanataka kukodishia wengine, kwa hiyo sisi mwisho wa siku, tukasema tutashughulika na wanaofanya biashara tu,"alisema.

"Kwa sasa tuna mkataba wa mwaka mmoja tu, haiwezekani watu wanawakodishia wenzao na wanaweka hadi kilemba (nyongeza ya bei), sisi tukasema tutatoa kwa bei elekezi ya soko linavyosema. Kuanzia Januari mosi, 2019 vibanda vyote vile vilikuwa ni mali ya Manispaa ya Moshi."

Mpaka sasa wafanyabiashara walioshindwa kumudu bei elekezi ya soko hilo, wamesharudisha maduka 27, kati ya maduka 153 yaliyoko katika jengo la biashara lililoko stendi kuu ya mabasi ya Moshi.

Kwa mujibu wa Mwandezi, manispaa hiyo ina uhuru na ina hiari ya kufanya biashara na yeyote yule ambaye yuko tayari kufuata taratibu za wakati uliopo. "Bei elekezi ilikuwa vibanda vya chini Shilingi 450,000 na vibanda katika ghorofa ya kwanza Shilingi 400,000, kwa wale ambao waliwekeza mwanzo tuliwapa kwa bei elekezi, lakini vile ambavyo vilibaki, wahusika waliviachia vibanda 27 na tulivitangaza na vilipata watu zaidi ya ile bei elekezi. Viko vilivyoombwa kwa Shilingi 500,000, 600,000 hadi 700,000 mpaka Sh. 900,000 tulipata na maombi tunayo mengi kabisa," amesisitiza mkurugenzi huyo.

Kabla ya Mwandezi kukomalia msimamo huo, juzi baadhi ya wafanyabiashara katika kituo kikuu cha mabasi cha Moshi mjini, walifunga maduka yao ya biashara yaliyoko katika jengo hilo, wakipinga kodi ya pango ya Sh.400,000 hadi Sh. 450,000.

Mwaka 2003, Manispaa ya Moshi iliingia mkataba na wananchi ambao walipenda kuwekeza katika kituo kikuu cha mabasi, ambapo pamoja na mambo mengine, mkataba huo ulisema wawekezaji wa kujenga viwanda vya biashara katika kituo hicho watafanya biashara bila malipo kwa miaka 15.

Kufikia Desemba 31, 2018, mkataba huo ulikuwa umefika ukingoni na manispaa ikadai muda huo ulitosha kurudisha gharama walizowekeza pamoja na faida.

# Mwarobaini uhaba vitabu wapatikana

**Na Paul William,** MWANGA

WILAYA ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, imezindua rasmi mkakati wake wa kukabiliana na tatizo la uhaba wa vitabu vya kiada, ziada pamoja na upungufu wa walimu katika shule za sekondari, kwa kuanzisha maabara maalum za kompyuta.

Uchache wa shule zenye maabara hizo za kompyuta, huchangia kuzorotesha elimu ya mtandao hapa nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, akizungumzia mpango huo wakati akikabidhi vyeti kwa walimu 116 wa shule za sekondari wa wilaya hiyo ambao wamejengewa uwezo wa kuendesha maabara hizo kufundishia, alisema kwa kiwango kikubwa elimu hiyo bado haijaweza kuwanufaisha wanafunzi wengi katika maeneo mbalimbali. Alisema ili kuendana na kauli mbiu ya serikali ya viwanda, walimu wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha wanafunzi wanaitambua teknolojia hiyo ya sasa kwa vitendo.

"Walimu mnajukumu kubwa la kuhakikisha maendeleo katika nchi yetu yanakuwa kwa kasi kubwa pamoja na kuhakikisha tunafikia azima ya Tanzania ya viwanda kwa kuzalisha wasomi wengi wanaoendana na teknolojia ya sasa," alisema Apson.

Kabla ya kuruhusiwa kuanza kutumika kwa maabara hizo, Mbunge wa Mwanga (CCM), Prof. Jumanne Maghembe, alisema sekta ya elimu imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa walimu na vitabu, hali ambayo imekuwa ikichangia kiwango cha ufaulu kushuka mara kwa mara. "Nia yangu katika kupambana na changamoto hizo, nimeamua kuanzisha maabara maalum ya kompyuta zitakazosaidia walimu kufundisha wanafunzi kwa kutumia kompyuta. Wanafunzi bado wana dhana potofu kwamba baadhi ya masomo magumu kama Hesabu na Kingereza, hivyo kupitia mfumo huu wa kompyuta utasaidia kuondoa dhana hiyo," alieleza Maghembe.

Zaidi alisisitiza: "Hata walimu wamekuwa wakikumbana na changamoto ya uhaba wa vitabu vya ziada na kiada, kwa hiyo kupitia mfumo huu wa kompyuta tutakuwa tumemaliza au kupunguza changamoto hiyo kwa kuongeza ufaulu."

Kupitia mpango huo, Prof. Maghembe ameeleza kwamba lengo lake ni kuwa na maabara 25 katika shule zote za sekondari zilizopo Wilaya ya Mwanga pamoja na kuwa na maabara mbili ambazo zitakuwa maalum kwa shule za msingi.

Akifafanua zaidi kuhusu maandalizi ya matumizi ya maabara hizo za kompyuta, Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya hiyo, Ashmun Mnzava, alisema mpaka sasa jumla ya walimu 116 wa shule za sekondari wamepatiwa mafunzo maalum ya kompyuta na kutambua jinsi ya kufundisha wanafunzi kupitia kompyuta.

Nipashe
Spotika
NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 18, 2019



KILICHOIBEBA SIMBA, KUIANGAMIZA YANGA UK.18

# PAMBANA...



## ISIKUPITE

HADI sasa Manchester City ndiyo yenye safu bora zaidi ya ushambuliaji kwenye Ligi Kuu England, ikiwa na uwezo wa kuipenya safu yoyote ya ulinzi kwenye ligi hiyo. Wamepiga mashuti 174 kwenye ligi. Pia ndio timu inayoongoza kwa kufunga mabao Ulaya msimu huu, huku wakiwa na mabao 114, mabao 47 zaidi ya wapizani wao Liverpool.

Lionel Messi akipata ushindani mkali kutoka kwa beki wa Real Valladolid, wakati Barcelona ikishinda 1-0 kwenye mechi ya La Liga iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou juzi. **HABARI UK. 28**

# KIFO CHANZO JEZI HIZI KUSTAAFISHA

**PARIS,** Ufaransa

KUSTAAFISHA namba ya jezi limekuwa jambo linalokubalika kwenye dunia ya soka ya sasa. Lakini ikitokea, inatokea kwa sababu nzuri tu. Mara nyingi hufanywa na klabu ili kutambua mchango wa mchezaji husika, lakini wakati mwingine ni njia ya kumbukumbu, baada ya kifo cha ghafla cha mchezaji husika.

Ustaafishaji wa namba ya jezi ulikuwa ukifanyika zaidi Marekani, lakini baada ya mwaka 1990, klabu nyingi zikaanza kufuata mfumo huo wa kustaafisha namba ya jezi kwa ajili ya kuwapa heshima wachezaji.

Hivi karibuni, dunia ya soka ilipatwa na mshituko baada ya kifo cha mshambuliaji wa Argentina, Emiliano Sala, ambaye alifariki baada ya kudondoka kwa ndege aliyokuwa akisafiria kutoka Ufaransa kwenda England. Sala alikuwa ameshakamilisha usajili wake wa kutoka katika Klabu ya Nantes ya Ufaransa kwenda Ligi Kuu ya England katika Klabu ya Cardiff kwa ada iliyoweka rekodi kwa klabu hiyo.

Ndege ndogo aliyokodi ilipotea saa chache baada ya kuruka. Sala alithibitishwa kufariki Februari 8, mwaka huu wakati mwili wake ulipokutwa katika mabaki ya ndenge hiyo chini ya bahari.

Klabu ya Nantes ikaamua kustaafisha jezi namba tisa (Na. 9) iliyokuwa inavaliwa na Sala. Nantes sio klabu pekee kustaafisha namba ya jezi baada ya kifo cha mchezaji.

Hapa tunaangalia matukio makubwa matatu yaliyosababisha klabu kuamua kustaafisha namba ya jezi kwa ajili ya heshima ya mchezaji ambaye alifariki dunia, twende sasa...

**3. Marc-Vivien Foé (23, Lyon, Man City na RC Lens)**

Marc-Vivien Foe alikuwa sehemu ya kikosi cha Cameroon kilichocheza kombe la Shirikisho la Fifa mwaka 2003. Juni 26, mwaka 2003, Cameroon ilikuwa inacheza na Colombia kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho. Katika dakika 72 ya mchezo huo, Foe alidondoka na baadaye kuthibitishwa kafariki hospitalini. Baadaye taarifa ya uchuguzi wa kifo chake ilisema Foe alifariki kutokana na matatizo ya moyo.

Kifo chake cha ghafla katika umri wa miaka 28 kilikuwa na mshituko mkubwa kwenye ulimwengu wa soka. Nyota wa Ufaransa, Thierry Henry, alishangilia bao lake kwa kutoa ishara mawinguni dhidi ya Misri kama kumbukumbu ya kifo hicho.

Wakati mauti yanamkuta Foe, alikuwa ni mchezaji wa Manchester City, akicheza kwa mkopo akitokea Lyon. Klabu yake ya Lyon, Manchester City na klabu yake ya utotoni Lens ziliamua kustaafisha jezi namba 23 moja kwa moja. Baadaye mchezaji wa kimataifa wa Cameroon, Jean Makoun alivaa jezi yenye namba ya Foe kwa ajili ya kumkumbuka rafiki yake.

**2. Cheick Tiote (24, Beijing Enterprise Group FC)**

Cheick Tiote alikuwa shujaa wa Newcastle wakati alipofunga bao la kusawazisha kwenye sare ya kukumbukwa dhidi ya Arsenal pale kwenye dimba la St James' Park. Bahati mbaya, tukio baya lilitokea kwa mchezaji huyo akiwa na umri wa miaka 30 alipodondoka wakati akiwa kwenye mazoezi na timu yake ya Beijing Enterprise Group FC.

Tiote alikimbizwa katika hospitali jirani na baadaye ilitangazwa kafariki dunia. Kisha madaktari walibainisha chanzo cha kifo chake kuwa ni tatizo la moyo.

Baada ya kifo hicho, klabu hiyo ya Ligi Kuu ya China, Beijing Enterprise Group FC (BG) ilistaafisha jezi namba 24, Juni 24, mwaka 2017, kwa ajili ya kumbukumbu ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, Cheick Tiote. Sherehe ya kustaafisha jezi hiyo ilifanyika kwa nusu ya mchezo wake dhidi ya Zhejiang Yiteng.

Katika uhai wake, Tiote aliichezea Klabu ya Tyneside. Aliichezea mechi 139 Newcastle katika misimu saba.

**1. Davide Astori (13, Fiorentina na Cagliari)**

Ni moja ya tukio lililoishitua dunia ya soka mwaka jana, wakati nahodha wa Fiorentina, Davide Astori alipothibitishwa kuwa amefariki dunia wakati akiwa amelala. Kufuatia tukio hilo, Fiorentina na Cagliari zilitangaza kustaafisha jezi namba 13 kwa ajili ya kumbukumbu ya kifo cha Davide Astori.

"Kwa heshima na kumbukumbu yake na kumfanya Davide Astori akumbukwe, Cagliari na Fiorentina zimeamua kwa pamoja kustaafisha jezi namba 13," hilo lilikuwa tangazo la klabu hizo walilolitoa kwa pamoja.

Sababu ya kifo chake ilitajwa kuwa ni matatizo ya moyo.


Davide Astori alikuwa beki wa kimataifa wa Italia ambaye aliichezea timu yake ya taifa mechi 174 na Klabu ya Cagliari aliichezea mechi 91 kabla ya kuhamia Fiorentina mwaka 2018.



Emiliano Sala

**JE, WAJUA?**

KATIKA mechi 35 zilizowakutanisha Lionel Messi (Barcelona) na Cristiano Ronaldo wakati akiwa Real Madrid, Messi ameweka rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi (22), huku Ronaldo akifunga mabao 19 tu.



# MICHEZO

## NJE YA UWANJA



## GRIEZMANN AIPIKU REKODI YA TORRES

**MADRID,** Hispania

ANTOINE Griezmann ameipiku rekodi ya Fernando Torres ya mchezaji namba tano mwenye mabao mengi katika historia ya Atletico Madrid.

Nyota huyo wa Ufaransa alimfikia nahodha huyo wa zamani wa klabu hiyo alipotupia kwa mkwaju wa penalti wakati wakishinda 3-1 katika mechi ya 'dabi' dhidi ya Real Madrid wiki moja iliyopita.

Griezmann alifunga bao lake la 130 kwenye mashindano yote katika klabu hiyo na la ushindi dhidi ya Rayo Vallecano Jumamosi, na kwa matokeo hayo yanaifanya Atletico kuwa nyuma kwa pointi tatu kutoka kwa vinara wa La Liga, Barcelona.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, anazidiwa tu na Luis Aragones (mabao 172), Adrian Escudero (169), Paco Campos (146) na Jose Eulogio Garate (136) kwenye urodha ya wafungaji wa wakati wote wa klabu hiyo.

Griezmann kwa sasa amefunga mabao nane katika mechi zake sita zilizopita ambazo walikutana na Rayo katika mashindano yote. Kadhalika, amewezesha ushindi wa 1-0 katika mechi tatu zilizopita kati ya hizo.




# COULIBALY ALIVYOPITIA NJIA NGUMU KAMA CHIRWA

**Na Adam Fungamwango**

ILIPOTOKA orodha ya wachezaji wa Simba kwenye mechi dhidi ya Al Ahly ya Misri, mashabiki na wanachama wa timu hiyo waliguna walipoliona jina la Zana Coulibaly, aliyepangwa kucheza beki wa kulia.

Ni mchezaji ambaye tangu atue kwenye klabu ya Simba hakuna chochote alichofanya ambacho wanachama na mashabiki wanajivunia nacho zaidi ya vituko mbalimbali kila kukicha.

Baada ya kuchapwa mabao 5-0 nchini Misri, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alionekana kukibadilisha kidogo kikosi chake Jumanne iliyopita. Zana alipangwa beki wa kulia badala ya Nicolaus Gyan na kumshangaza kila mmoja.

Hata hivyo, beki huyo naye raia wa Burkina Faso alimshangaza kila mtu alipocheza mechi hiyo, dhidi ya timu hiyo kubwa kabisa barani Afrika kwa kiwango cha juu mno.

Zana ndiye aliyepiga majalo iliyomkuta John Bocco, kabla ya kumtengea Meddie Kagere na kuujaza wavuni, likiwa ni bao pekee kwenye mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi, Simba ikishinda 1-0.

Alifanya majaribio kadhaa ya hatari, akipiga krosi zilizoleta hatari, pamoja na kupambana na wachezaji wenye nguvu wa Al Ahly, akifanikiwa kuwashinda.

Haikushangaza mara baada ya mechi kumalizika, mashabiki wengi uwanjani walikuwa wakiliimba jina lake. Kwenye basi la wachezaji, mashabiki walionekana kumfuata dirishani na kumpongeza.

Kwenye vibanda vya kuonyesha mpira, mitaani na kwenye mitandao ya kijamii, mbali na ushindi wa Simba, stori ilikuwa ni kiwango kikubwa kilichoonyeshwa na beki huyo ambaye tayari wengi walikuwa wameshaanza kumdharau.

Wapo walioona kama alibahatisha au siku hiyo ameamka vizuri, lakini kwenye mechi dhidi ya Yanga alipangwa tena na kuonyesha kiwango kizuri kama dhidi ya Al Ahly na kuwasuta wote waliokuwa wakimbeza.

Akizungumza baada ya mechi hizo mbili, aliwashukuru mashabiki wa Simba ambao walionyesha kumuunga mkono wakati akiendelea kurejea katika kiwango chake.

Mara tu baada ya mechi, Zana aliwafuata mashabiki wa Simba na kuwaonyesha ishara ya shukurani na baadaye kusema, walimvumilia na sasa ameanza kupata kiwango chake.

Afisa Habari wa Simba, Haji Manara, aliwashauri mashabiki wa soka nchini kuwa na tabia ya uvumilivu kwa wachezaji wanaokuja nchini.

"Hata George Weah alipopelekwa Ufaransa kwenye klabu ya Monaco alibezwa sana, ilibaki kidogo arudi Afrika kama si kocha Arsene Wenger. Leo kuna maswali huko kwenu juu ya uwezo wa beki huyu mwenye mbwembwe nyingi?"Alihoji Manara.

Hawa ni baadhi ya wachezaji waliokuja nchini na kuonekana 'mabomu' , lakini baadaye wakawa moto wa kuotea mbali na kushangiliwa, kuimbwa kila kona.

**Emmanuel Okwi-Simba**

Alifika Simba mwaka 2009 akitokea Uganda kwenye klabu ya SC Villa na mechi yake ya kwanza ilikuwa ya Simba Day dhidi ya URA. Simba ikachapwa bao 1-0. Hakuonekana kwenye kiwango kizuri kuliko mwenzake aliyesajiliwa naye Joseph Owino.

Wanachama na mashabiki wa Simba walilalamika kwa viongozi kuwa badala ya kuleta wachezaji hasa waliyekuwa wanamhitaji wakati huo Brian Umony, wao wameleta 'mtoto wa shule'. Leo hakuna asiyemjua Okwi na shughuli yake Afrika Mashariki na Kati nzima.

**Donald Ngoma-Yanga**

Straika huyu raia wa Zimbabwe ambaye kwa sasa anaichezea Azam, alisajiliwa na Yanga mwaka 2015 akitokea FC Platinum ya Zimbabwe.

Awali hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida. Alionekana mzito hana kasi. Alikuwa akibezwa na mashabiki wa Simba kila anapopata mpira uwanjani.


Baada ya kuzoea mazingira ya soka la Bongo ameondokea kuwa ni mmoja wa mastraika hatari kiasi cha kuogopewa na hata waliokuwa wakimbeza. Kwa misimu aliyocheza Tanzania, amefunga mabao mengi akiwa na timu za Yanga na Azam anayochezea kwa sasa.

**Obrey Chirwa-Yanga**

Alisajiliwa na Yanga Juni 2016 kipindi cha dirisha dogo na kucheza mechi 11 bila kufunga bao. Hata uchezaji wake uwanjani haukuwa wa kuridhisha, kiasi cha kuwakera hata Yanga wenyewe. Mmoja wa wanachama nguli wa Yanga, Ibrahim Akilimali alikuwa mmoja wa watu waliodai anakula pesa za bure.

Ilibaki kidogo raia huyo wa Zambia arejeshwe kwenye timu yake ya zamani FC Platinum ya Zimbabwe ili nafasi ya mchezaji wa kigeni ijazwe na mwingine, lakini mambo yalienda kombo na akabaki. Ikawa ni nafasi yake ya kuonyesha kuwa yeye ni nani. Alibadilika na kuwa straika tegemeo wa Yanga na hasa wakati huo Ngoma alikuwa ameshaanza kuwa majeruhi na kuchangia timu hiyo kutwaa ubingwa. Kwa sasa anaichezea Azam FC akiwa na swahiba wake Ngoma.

## Extra Time




# Wa5 wanaotakiwa kutua Real Madrid

**MADRID,** Hispania

TUNAWEZA kusema Real Madrid wameendelea kuwa na ndoto mbaya msimu huu; kwa sasa wamepitwa pointi sita na vinara wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona.

Pia wanakabiliwa na ukame wa muda mrefu zaidi wa kufunga mabao katika historia ya klabu hiyo, huku wakiwa wamecheza dakika 481 bila bao.

Pia imekuwa ni miaka mitato tangu Los Blancos hao walipomsajili mchezaji ambaye angeweza kufiti kwenye sera yao ya 'Galáctico', wa mwisho akiwa James Rodríguez mwaka 2014.

Huku Cristiano Ronaldo akiwa ameondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita na hakuna aliyeletwa kuziba pengo lake. Madrid watakuwa na nafasi ya kuongeza nyota kadhaa kipindi kijacho cha majira ya joto.

Licha ya kushinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwamo msimu uliopita, Real Madrid inaonekana ni kama imepoteza dira.

Pamoja na kumpoteza Ronaldo na kutopata mrithi wake, kuna sababu kadhaa kwa hilo. Sababu ya kwanza ni kwamba wachezaji ambao ni nguzo kama vile Luka Modric, Sergio Ramos, Marcelo na Benzema kwa sasa wapo kwenye umri wa miaka 30 na wameanza kuchoka, au hawawezi kucheza mechi 50 kwa msimu.

Sababu nyingine ni kutokuwa na kikosi kipana. Ilikuwa wazi kwamba msimu wa hivi karibuni ambao Madrid walikuwa na mafanikio makubwa zaidi ni ule wa 16/17, ambapo walikuwa na uwezo wa kuchezesha timu mbili tofauti. Msimu huo, kwenye ligi na Kombe la Hispania ilicheza timu nyingine tofauti kabisa.

Hata hivyo, kikosi hicho bado kilikuwa na wachezaji kama Alvaro Morata, James Rodriguez na Asensio. Morata na Rodriguez wameondoka.

Bila ya wachezaji hawa nguzo, Madrid imekuwa na wakati mgumu zaidi kwenye safu ya ushambuliaji.

Madrid imekuwa kwenye wakati mgumu mwishoni mwa msimu uliopita na msimu huu, wameruhusu mabao mengi ya kufungwa na wao kufunga machache kuliko wapinzani wao Barcelona.

Madrid imeruhusu mabao 27 kwenye La Liga, huku Barca ikiruhusu mabao 23, lakini wamefunga mabao 40, huku Barcelona wakifunga 60. Hilo limewaacha wao kuwa na tofauti ya mabao 13 baada ya kucheza mechi 23, wakati Barca wana tofauti ya mabao 37.

Karim Benzema amekuwa katikati ya lawama kwa mashabiki wa Madrid kutokana na kutokuwa na kiwango cha kufunga mara kwa mara.

Msimu uliopita Benzema alifunga mabao matano kwenye ligi, sawa na kiungo, Toni Kroos.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao Real Madrid inatakiwa kuwasajili wakati wa kipindi kijacho cha majira ya joto ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi.

**4. Matthijs de Ligt**

Barcelona tayari imetangaza kumsajili nyota wa Ajax, Frenkie de Jong ambapo usajili wake ulithibitishwa wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari na atatua pale kipindi cha majira ya joto. Ripoti zinasema kwamba Barca pia wanapanga kumsajili patina wake, Matthijs de Ligt kipindi cha majira ya joto ili atue hapo Camp Nou.

Kama Real wataweza kuingilia kati kwenye dili hili na kumsajili mchezaji huyo, wataongeza makali kwenye kikosi chao na kuifanya safu yao ya ulinzi kuwa imara zaidi. Kwani watakuwa wamepata beki wa kati kijana na mwenye kipaji. Sergio Ramos kwa sasa ana umri wa miaka 32 hataweza kwenda mbali. De Ligt anaweza kuwa mbadala wake halisi.

Historia ya De Ligt inafanana na Ramos, kwa staili ya uchezaji na namna anavyoweza kuipanga safu yake ya ulinzi. De Ligt ana uwezo mkubwa zaidi wa kuondoa mpira kwenye eneo lake la hatari.

De Ligt msimu huu umekuwa wa kuvutia zaidi kwake, akitoa pasi zenye uhakika kwa asilimia 91.4. Uwezo kama huu utaweza kuisaidia Madrid kwenye kutawala mchezo, na pia ana uwezo mkubwa wa kutengeneza mashambulizi hatari kwa timu pinzani. De Ligt ndiye aliyeweza kumzuia kabisa Robert Lewandowski, wakati Ajax ikitoka sare ya bao 1-1 na Bayern Munich pale kwenye dimba la Allianz Arena.

**3. Eden Hazard**

Wakati huu kila kitu kinaonyesha kwamba, Hazard atajiunga na Madrid. Inaonyesha kwamba haipiti wiki bila ya Hazard kutoa kauli kuhusu Madrid. Na kipindi cha majira ya joto kinaonekana wazi kwamba usajili wake utafanyika. Huku yeye mwenyewe akionyesha wazi kwamba ana nia kubwa ya kujiunga na Madrid. Cristiano Ronaldo kwa sasa ameondoka, na kuacha pengo kubwa kwenye winga ya kushoto, pamoja na kukosekana kwa mchezaji mbunifu. Hazard pia anafiti kwenye kikosi cha Galactico kutokana na ubora wake.

Kwa uwapo wa Hazard, Madrid itakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutengeneza mashambulizi kutoka winga ya kushoto.

Hazard amekuwa na wakati mzuri zaidi kwenye Ligi Kuu ya England, akifunga mabao 12 na kutoa pasi za mwisho 10 msimu huu. Pia ana uwezo mkubwa wa kucheza kama mshambuliaji pekee. Kama atatua pale Real Madrid kutaifanya safu yake ya ushambuliaji kuwa hatari zaidi.

Huku mkataba wa Hazard pale Chelsea ukiwa unaelekea ukingoni na akiwa ameonyesha wazi kwamba hana mpango wa kuongeza, hii ni nafasi nzuri zaidi kwa Madrid.

**2. Neymar**

Huyu ndiye anaweza kuwa mchezaji sahihi zaidi wa kurithi mikoba ya Cristiano Ronaldo pale Real Madrid. Nyota huyo wa Brazil kwa kiasi kikubwa anafanana kwa staili yake ya uchezaji na Ronaldo hasa kwenye upachikaji wa mabao. Jambo muhimu zaidi kwa Madrid ni kwamba, mchezaji huyu ndiye pekee anaweza kuvaa vizuri na kufiti kwenye viatu vya Ronaldo. Kuanzia kwenye matangazo ya biashara hadi dimbani anaweza hata kumzidi Ronaldo kwenye soko la biashara. Neymar amecheza kwenye Ligi ya Hispania akiwa na Barcelona hivyo anafiti kabisa kwenye Galáctico na kama Madrid wataweza kuipata saini yake kipindi cha majira ya joto, watakuwa wamefanya usajili bora zaidi kwa wakati walionao.

Neymar amekuwa na msimu mzuri kule Ufaransa katika Ligi Kuu, kwani hadi sasa amefunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho sita kwenye mechi 13 alizocheza. Unaweza kumwita ni mchezaji aliyekamlika. Neymar ataweza kuisaidia Madrid kwenye umiliki wa mpira.

Uwezo wa Neymar si wa kuutilia shaka hata kidogo, kwani tayari ameshafunga jumla ya mabao 289 kwenye ngazi ya klabu na mabao 60 kwa nchi yake na pia alishinda mataji matatu akiwa pale Barcelona na kumfanya ashike nafasi ya tatu katika tuzo ya Ballon d'Or.

**1. Kylian Mbappe**

Karibia kila kitu kilichosemwa kuhusu Neymar kinaweza kufanana na Kylian Mbappe. Yeye ni mfamle wa dimba kwa sasa. Tayari katika umri wake wa miaka 20 ameshashinda Kombe la Dunia. Hivyo, kama Real Madrid watamsajili Mbappe watakuwa wamemaliza kabisa tatizo la ufungaji mabao kwenye kikosi chao.


Mbappe amekuwa na msimu wenye mafanikio zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu huu, huku akiwa amefunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi zake 16 alizocheza.

Mbappe ataongeza chachu zaidi kwenye safu ya ushambuliaji ya Madrid. Na kitu kizuri zaidi kwa Real Madrid kufanya usajili wa Mbappe ni umri wake. Kwani kwa umri aliona hivi sasa kuna nafasi kubwa zaidi ya kumshuhudia akiendelea kucheza kwa kipindi cha miaka 13 ijayo.

Mbappe ndio mrithi sahihi wa Ronaldo na ambaye anaweza kufuata nyayo zake kwenye mafanikio.

## NUKUU


"Kama ulivyokwisha kusikia, nimekubaliana mkataba wa awali na Klabu ya Soka ya Juventus. Nilitaka kutoa taarifa ya binafsi kwa mashabiki wote wa Arsenal ambao wamekuwa waaminifu sana na wanaounga mkono. Ulinipokea mimi kama kinda na umekuwa nami hapo nikiwa katika kiwango cha chini na cha juu kwa muda wangu wote klabuni hapo. Ni kwa moyo mzito kwamba ninaondoka baada ya miaka 11 ya kushangaza kaskazini mwa London. Asante," **Aaron Ramsey ambaye anayejiandaa kutua Juve majira ya joto.**




"Siwezi kufanya chochote kuhusu Alexis [Sanchez], anahitaji kujibidisha mwenyewe kama tunavyojua kuna wachezaji wenye ubora pale, ukweli Jesse [Lingard] na Anthony [Martial] wanacheza vizuri," kocha Ole Gunnar Solskjaer, **akieleza kutofurahishwa na uwezo wa Sanchez aliouonyesha kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita dhidi ya PSG**



"Hapa nilitambua soka la Kiingereza ni zaidi kuliko hapo awali na kwa nini kombe hili ni maalum kwa timu katika hali hiyo - wanatumia nguvu zao na ndiyo sababu kombe mara zote lina mshangao mkubwa," **kauli ya Pep Guardiola baada ya Manchester City juzi kuichapa Newport County mabao 4-1 na kutinga robo fainali ya Kombe la FA.**






Mfungaji wa bao pekee Simba, Meddie Kagere (kulia), akishangilia wakati timu hiyo iliposhinda 1-0 dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Taifa juzi. Pembeni ni Emmanuel Okwi.

# KILICHOIBEBA SIMBA KUIANGAMIZA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

ALIKUWA ni yule yule Meddie Kagere, straika wa Kinyarwanda aliyefunga bao pekee dhidi ya Al Ahly akipokea pasi ya mwisho kutoka kwa nahodha John Bocco baada ya kufanya hivyo Jumanne iliyopita wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Waarabu hao wa Misri, na juzi tena wawili hao wakarudia mchezo ule ule Simba ikiwachapa watani wao wa jadi, Yanga.

Kagere alifunga bao hilo dakika ya 71, akimalizia pasi kutoka kwa nahodha wa timu hiyo, John Bocco na Simba kuondoka na ushindi wa bao 1-0. Baada ya kuchapwa mechi hiyo, Yanga imehitimisha misimu mitatu bila kuifunga Simba.

Mara ya mwisho Yanga kuifunga Simba ilikuwa ni Februari 20, 2016, ikiwa ni Ligi Kuu msimu wa 2015/16, iliposhinda mabao 2-0, yaliyowekwa wavuni na Donald Ngoma na Amissi Tambwe.

Kwa ushindi huo, Simba imechukuwa pointi nne kwa Yanga, kwani kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza timu hizo zilitoka sare katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam bila kufungana mechi ikichezwa Septemba 30, mwaka jana.

Pia imerejea kwenye nafasi yake ya tatu kwa kufikisha pointi 39, ikipitwa na timu mbili juu, Azam ikiwa ya pili kwa pointi 49 na Yanga ikiendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 58.

Kwa upande wa Yanga, pamoja na kipigo hicho, bado inaendelea kuongoza, lakini ikiwa imepoteza mechi mbili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kama ilivyo kwa Azam FC.

Takwimu zinaonyesha kuwa ni Simba pekee kwenye Ligi Kuu iliyopoteza mechi moja tu.

Na hapa ni sababu iliyofanya Simba kuibuka kidedea katika mechi hiyo ya juzi Uwanja wa Taifa.

Tofauti na mzunguko wa kwanza ilipolazimishwa sare bila kufungana dhidi ya Yanga, safari hii Simba ilionekana kuwa vizuri zaidi kutokana na kwanza wachezaji wake kuelewana, ambapo hapo kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza ilikuwa na wachezaji wapya na wa zamani ambao walikuwa bado hawajaelewana vizuri.

Pili bado kulikuwa na fukuto la kutoelewana kwa Kocha Mkuu, Patrick Aussems na msaidizi wake Masoud Djuma, sakata ambalo linadaiwa liliingia hata kwa wachezaji.

Safari hii Simba iliingia pia ikiwa imepata mechi nyingi ngumu za kimataifa kuanzia kwenye Ligi ya Mabingwa hatua za awali hadi kwenye makundi, kitu ambacho kinaonekana kuwa wachezaji wake wamekomaa zaidi.

**Yanga iliingia kivingine kabisa**

Pongezi kubwa ziliendee benchi la ufundi la Yanga kwani kama wangecheza kama walivyofanya mzunguko wa kwanza wangefungwa mabao mengi.

Pamoja na kipindi cha kwanza kuonekana kuzuia zaidi, lakini ilibadilika kipindi cha pili na kufanya mashambulizi kadhaa ambayo yaliwapa wakati mgumu mabeki wa Simba.

Yanga ilijaza viungo wakabaji wengi, lakini baadhi yao kama Feisal Salum 'Fei Toto' na Papy Tshishimbi walikuwa wakibadilika na kuwa viungo washambuliaji wanapoanza kufanya mashambulizi, hivyo walikuwa wakifanya kazi mbili kwa wakati mmoja.

**Chama aliikosesha Simba ushindi mnono**

Kwa sasa injini ya Simba kupeleka mashambulizi upande wa wapinzani ni Clatous Chama.

Hata hivyo, kwenye mechi dhidi ya Yanga hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida na kuwafanya viungo wa timu pinzani kumdhibiti kwa urahisi.

Kama Chama angekuwa kwenye kiwango kilichozoeleka, inawezekana kabisa Simba ingeweza kupata bao hata kipindi cha kwanza na hali ingekuwa ngumu kwa Yanga.

Shukrani kwa Hassan Dilunga, kwani alipoingia Simba ilianza kurejea kwenye kiwango chake kilichozoeleka na kupeleka mashambulizi mfululizo, hadi lilipopatikana bao pekee.

**'Sub' ya Ajibu ilimaliza mechi**

Mabadiliko yaliyofanywa na Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera ya kumtoa nahodha Ibrahim Ajibu na kumuingiza Mohamed Banka yaliyonekana ni kama yamemaliza mechi yenyewe. Nia ya Zahera ilikuwa nzuri tu kwani mara nyingi Ajibu huchoka kabla ya dakika 90 na alikuwa anataka mtu mwingine aliyekuwa na pumzi na mbunifu kama Ajibu.

Pamoja na hayo Banka hakuwa kwenye kiwango chake kilichozoeleka kwa sababu hajacheza muda mrefu.

Ajibu ni mchezaji ambaye hata kama akiwa amechoka, lakini huwa na umuhimu mkubwa akiwa uwanjani, kutokana na ubunifu wake, pasi zake za mwisho na mipira iliyokufa.

Pia anapokuwa na mpira, mabeki wa timu pinzani wanakuwa kwenye wakati mgumu. Ndiyo maana alipotoka, mabeki wa Simba ni kama walikuwa wamepumzika hivi.

**Yanga ilijitia presha yenyewe**

Kitendo cha basi la Yanga kwenda uwanjani bila wachezaji, huku wakiwa wamepanda kwenye gari lingine, ilionekana kabisa kuwa viongozi wa timu hiyo walikuwa kwenye shinikizo kali na wachezaji wao kwa ajili ya mechi hiyo.


Mmoja wa kiongozi wa Yanga alisema kuwa walifanya hivyo kwa ajili ya kwatoa kwenye mchezo wapinzani wao, lakini kumbe walijitoa wenyewe mchezoni.

Wakati mwingine kufanya vitu tofauti kwenye mechi hiyo, kunawafanya hata wachezaji kupata presha na kuona kuwa ni mechi tofauti na nyingine.

Ukisikiliza maneno waliyokuwa wakiongea na kuandika kwenye mitandao ya kijamii, yalionyesha kuwa waliihofia sana mechi hiyo, hivyo kuwapa hofu wachezaji wao pia.


**NAJUA WAJUA**

WAKATI Arsenal ikishinda 2-1 dhidi ya Cardiff wiki moja iliyopita, beki Stephan Lichtsteiner ilikuwa ni mechi yake ya 400 kwenye ligi kubwa tano bora Ulaya, na ilimfanya kuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri wa miaka 35+ kuanza mechi ya EPL kwa Arsenal (akiwa na miaka 35 na siku 13) tangu Sol Campbell alipocheza dhidi ya Fulham akiwa na umri huo Mei 2010.



## MAKALA

# SABABU 3 MAN CITY BINGWA EPL 2018/19




**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City ilikuwa na mwanzo mzuri wa msimu huu na kwa kila mtu hilo halikuwa jambo la kushangaza. Hayo ni matokeo ya kufanya vizuri zaidi msimu uliopita ambapo walivunja rekodi kadhaa na kulitwaa taji la Ligi Kuu ya England. Vijana hao wa Pep Guardiola hawakuwa na mzaha.

Walicheza soka la kuvutia na rahisi kwa kila mmoja kuweza kumiliki mpira. Baada ya kutumia fedha nyingi kwenye usajili, timu yao imeonekana kuwa yenye uwiano sahihi. Hasa kwa kufanya usajili wa wachezaji wakubwa Ulaya.

Man City ilifungwa mara mbili dhidi ya Chelsea na Crystal Palace kabla ya Krismasi na baadaye dhidi ya Leicester City. Hilo likawafanya wawe chini ya Liverpool, ambao kwa sasa wana pointi sawa kileleni mwa msimamo.

Hata hivyo, City ina kikosi ambacho huwa hakikati tamaa na mara zote kinapigana kuhakikisha kinashinda katika kila mchezo. Mbio za ubingwa zinakaribia mwisho, huku Spurs nao wakiwakimbiza. Manchester City bado ndio wenye nafasi kubwa ya kulitwaa taji hilo kwa mara ya pili mfululizo ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 10.

Hapa tunaangalia sababu kwa nini Man City watalitwaa tena taji hilo...

**1. Safu bora ya ushambuliaji EPL**

Manchester City ina safu bora zaidi ya ushambuliaji kwenye Ligi Kuu. Safu yao ina uwezo wa kuipenya safu yoyote ya ulinzi kwenye Ligi. Wamepiga mashuti 174 kwenye ligi. Pia ndio timu inayoongoza kwa kufunga mabao Ulaya msimu huu, huku wakiwa na mabao 114, mabao 47 zaidi ya wapizani wao Liverpool.

Kikosi hicho kina safu nzuri zaidi ya ushambuliaji ndani ya dimba na nje ya dimba. Uwepo wa majina makubwa kama Sergio Aguero, Raheem Sterling, Leroy Sane na Kevin De Bruyne kunaipa nafasi nzuri zaidi ya kujitanua. Kiungo na winga David Silva mara zote amekuwa akifanya kazi kubwa ya kutengeneza mashambulizi.

Ukiangalia pale benchi, kuna Riyad Mahrez na Gabriel Jesus ambao wapo tayari kutoa msaada wowote. Hilo linawapa wakati mzuri zaidi wa kushinda katika kila mchezo.

**2. Uzoefu wa kushinda taji**

Vijana hawa wa Pep Guardiola wana nafasi kubwa dhidi ya wapinzani wao kwenye suala la uzoefu. Faida kubwa ni kwamba, wameshinda taji lililopita, huku Liverpool hawana chochote. Imeshuhudiwa mara nyingi kwenye Ligi Kuu kwa siku za nyuma timu iliyoongoza kwa muda mrefu, mwisho wa siku inajikuta inaangukia pua. Liverpool pia wamekuwa wahanga wa tatizo hilo.

Manchester City imeonyesha kwamba, kila wanapopata nafasi huwa hawafanyi masihara. Mfano mzuri ni miaka nane iliyopita. Walishinda taji la Ligi Kuu kwa bao la dakika za mwisho la Aguero.

Mara zote wamekuwa wepesi wa kurudi mchezoni hata kama wamefungwa. Kikosi cha Liverpool bado hakijawahi kukumbana na kitu kama hicho. Jurgen Klopp kwa siku za hivi karibuni amekuwa akizungumzia uwezo wa timu yake kutuliza presha pale inapofungwa na hilo linawafanya kuwa kwenye wakati mgumu zaidi.

**3. Ubora wa Guardiola**

Manchester City bila shaka wana kocha bora zadi duniani, kwani Pep Guardiola, amekuwa na maono mazuri na uwezo wa kuubadilisha mchezo kuwa wa kuvutia.


Timu yake imekuwa na mafanikio kila sehemu aliyopita, kuanzia Barcelona na Bayern Munich. Amelifanya soka kuwa katika daraja la juu zaidi katika kila klabu aliyofundisha kwenye ligi tofauti.

Alikuwa na mwanzo mgumu England wakati alipoanza kazi yake ya ukocha bila taji lolote msimu wake wa kwanza. Akatengeneza kikosi cha vijana wenye vipaji na hilo limemsaidia. Kuanzia hapo timu yake imeonekana kuwa bora zaidi.

Ameiwezesha timu yake kutumia vizuri uwanja wake wa nyumbani wa Etihad na kuhakikisha inaibuka na ushindi. Amekijenga kikosi cha kupambana katika kila mchezo na hata wachezaji wanaonekana kufurahia kucheza chini yake. Hivyo kwa namna yoyote ubora wa Guardiola una mchango mkubwa zaidi kwa kikosi cha Manchester City. Kama akishinda taji la Ligi Kuu msimu huu, itakuwa ni mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 10 timu kushinda taji mara mbili mfululizo kwenye Ligi Kuu England.

**NDANI YA 18**

SERGIO Aguero ameifungia Man City mabao nane kwenye Ligi Kuu England kwa mwaka 2019 - ambayo ni mara mbili kuliko yaliyofungwa na mchezaji yeyote kwenye ligi hiyo huku pia yakiyapiku mabao ya timu 11 kwa mwaka huu ikiwa ni pamoja na Chelsea iliyotupia mara saba.





TUNAWEZA kusema Real Madrid wameendelea kuwa na ndoto mbaya msimu huu; kwa sasa wamepitwa pointi sita na vinara wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona. Pia wanakabiliwa na ukame wa muda mrefu zaidi wa kufunga mabao katika historia ya klabu hiyo, huku wakiwa wamecheza dakika 481 bila bao..

Uk. 16-17

# SOKONI KUNAWAHUSU WANNE HAWA BARCA



**BARCELONA,** Hispania

KWA viwango vyote, huu umekuwa msimu mzuri zaidi kwa Barcelona. Wakiongoza msimamo wa ligi kwa tofauti ya pointi sita na wapinzani wao, Real Madrid ambao wapo nafasi ya pili, na ni wazi kwamba Blaugrana hao wana nafasi nzuri ya kulitetea taji lao.

Kwingineko wapo kwenye nafasi nzuri ya kuweka rekodi ya kulitwaa kwa mara ya tano mfululizo Kombe la Mfalme [Copa del Rey], ingawa watatakiwa kushinda mchezo wao wa pili wa nusu fainali wa El Clasico pale katika dimba la Bernabeu ili watinge fainali. Ligi ya Mabingwa Ulaya pia ipo kwenye nafasi yao, wiki hii watacheza na Lyon kwenye hatua ya mtoano wa timu 16.

Nafasi yao hiyo kwa kiasi kikubwa imechangiwa na mshambuliaji na nahodha wao, Lionel Messi, huku nyota huyo wa kimataifa wa Argentina akionekana wazi kwamba anapania zaidi msimu huu.

Hata hivyo, uwezo wa Messi unaongezewa chachu zaidi na wachezaji wenzake kama Sergio Busquets, Gerad Pique na Luis Suarez huku pia kukiwa na damu changa kama Clement Lenglet, Ousmane Dembele na Arthur Melo.

Hata hivyo, katika makala haya, tunawaangalia wachezaji wanne ambao wanatakiwa kuuzwa msimu ujao.

**1. Philippe Coutinho**

Baada ya majadiliano ya muda mrefu kati ya Coutinho na Liverpool, Barcelona walimsajili Januari 2018 kwa ada iliyoweka rekodi kwa klabu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil aliwasili hapo huku kukiwa na matarajio makubwa ya kuwa mrithi sahihi wa kiungo Andres Iniesta na alianza kwa kuwa na mafanikio ya kuvutia. Kwani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alifunga mabao 10 katika mechi 22 alizowachezea miamba hao wa Katalunya kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, mambo yanaonekana kutokwenda sawa kwa upande wake, kwani kwa sasa anaonekana wazi kutokuwa na nafasi katika kikosi cha kwanza cha kocha, Ernersto Valverde, ambaye amekuwa akiwatumia washambuliaji watatu mbele, Messi, Suarez na Dembele.

Kiwango cha Coutinho kinaonyesha ishara kwamba, uwezekano wa kuendelea kucheza katika kikosi hicho kwa siku za usoni haupo, kwani nafasi yake ni ndogo.

Ripoti zinabainisha kwamba, klabu ipo tayari kusikiliza ofa yoyote kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil na ni wazi kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

**2. Malcom**

Huu ulikuwa ni usajili uliojaa utata wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, Malcom tayari alikuwa akionekana kwamba safari yake inaelekea kule AS Roma akitokea Bordeaux huku klabu hiyo ikitangaza kabisa kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Twitter kumkaribisha mchezaji huyo kwa mashabiki wao.

Lakini katika hali ya kushangaza, Barcelona 'walimteka' juu kwa juu na baada ya hapo kila kitu kikawa historia.

Malcom alikuwa mmoja wa wachezaji vijana waliokuwa wanawaniwa zaidi na klabu za Ulaya baada ya kuwa na mafanikio makubwa kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa na alitarajiwa kwamba angekuwa na mafanikio makubwa pale Barcelona.

Hata hivyo, mambo yamekwenda tofauti, kwani Ousmane Dembele amekuwa kwenye kiwango kizuri zaidi na hivyo kupata nafasi ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza, huku Malcom akishindwa kuonyesha kiwango chake Barcelona tangu alivyotua.

Hadi sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amecheza mechi 14 kwenye mashindano yote, akifunga mabao matatu, wakati akiwa bado hajaweza kuanza kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa au La Liga.

Ni wazi kwamba, Malcom hana maisha marefu pale kwenye dimba la Nou Camp na hivyo utakuwa wakati sahihi kwake kuuzwa mwishoni mwa msimu ili kwenda kujaribu maisha sehemu nyingine.

**3. Denis Suarez**

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 25, amekuwa na maisha yasiyo na mafanikio Barcelona hadi sasa. Kwa mara ya kwanza aliitumikia klabu hiyo kuanzia mwaka 2013 hadi 2015, lakini akicheza katika kikosi cha pili, kabla ya kuhamia kule Villarreal.

Kiwango chake akiwa Villarreal kikawashawishi Barca na wakamrudisha mwaka 2016, lakini tangu hapo hakuwa na mchango wowote kwa timu na alishindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza.

Katika misimu yake mitatu na klabu hiyo, Denis Suarez amecheza jumla ya mechi 71 kwenye mashinano yote, akifunga mabao nane kabla ya kupelekwa kwa mkopo Arsenal Januari mwaka huu.

Kiukweli hakuwa sehemu ya kikosi cha kwanza cha Barcelona hata kumpa mkataba mpya lilikuwa ni jambo la kushangaza. Hata hivyo, ni wazi kwamba uwezekano wa kurudi tena Barcelona ni mdogo na kama atakuwa na kiwango kizuri hapo Arsenal anaweza kuuzwa hapo hapo kwa mkataba wa kudumu.

**4. Thomas Vermaelen**

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 33, alisajiliwa kutoka Arsenal mwaka 2014 kwa ada ya pauni milioni 15, baada ya kuwatumikia 'Washika Bunduki' hao kwa misimu mitano.

Usajili wake wa kutua kwa miamba hao wa Catalunya ulikuwa wa hatari, hasa kutokana na historia yake ya kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara akiwa pale Arsenal. Pia tangu ametua hapo Barcelona amendelea kuwa na matatizo ya majeraha na alikuwa nje ya dimba kwa kipindi cha zaidi ya mara 12.

Vermaelen ameichezea Barcelona mechi 50 katika mashindano yote kwa misimu minne aliyokaa hapo (ingawa msimu wa 2016/17 alipelekwa kwa mkopo kule AS Roma).

Msimu huu, amecheza mechi nane tu katika mashindano yote, hivyo ni wazi kwamba Barcelona hawataweza kuendelea naye hasa kutoka na uwapo wa mchezaji kijana Clement Lenglet, Gerard Pique na Samuel Umtiti.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelguji unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto, na hivyo inakuwa kazi rahisi kwa wao kumruhusu kuondoka akiwa kama mchezaji huru.

**USILOLIJUA**

ENDAPO Manchester City itatwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu, itakuwa klabu ya kwanza kubeba taji hilo mara mbili mfululizo kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita.





## UVCCM wapewa jukumu la jamii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoani Mbeya, umewataka wanachama wa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM) katika vyuo vikuu nchini kuwa chachu ya maendeleo nchini kwa kushiriki katika shughuli za kijamii.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, katika Kongamano lililoandaliwa na UVCCM tawi la Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya na kushiriki kufanya usafi katika Hospitali ya Mkoa wa Mbeya kama sehemu ya kuadhimisha miaka 42 ya kuzaliwa kwa chama hicho.

Mwakasole aliwataka vijana hao kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ili kuonyesha tofauti kati ya chama hicho na vyama vya upinzani ambavyo wanachama wake wanapinga kila kitu kinachofanywa na serikali.

Aliwataka vijana hao kuachana na chuki za kisiasa kati ya CCM na vyama vya upinzani na kuwabeza wale wote wanaopinga maendeleo ya taifa katika sekta mbalimbali.

"Vijana mnapaswa kutambua ninyi ni chachu ya maendeleo katika serikali ya awamu ya tano, ni jukumu lenu kutumia sera katika kuleta maendeleo ya kweli, mwendelee kushiriki shughuli za kijamii kama Rais wetu Dk. John Magufuli anavyofanya," alisema Mwakasole.

Mwenyekiti wa UVCCM tawi la Mzumbe, Asini Ngonyani, alisema kwa kutambua wajibu wao ndani ya jamii wamejiwekea mipango mikakati ya kushirikiana na jamii katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika kuunga mkono jitihada za viongozi wa chama na serikali ya awamu ya tano.

Alisema kipindi hiki sio cha kejeli bali ni kuonyesha vitendo katika utekelezaji wa sera na katika kusimamia uboreshaji wa sekta za afya, elimu na miundombinu itakayoleta tija kwa wananchi.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa, Dk. Glory Mbwile, alisema utaratibu uliowekwa na wanavyuo wa kufanya usafi katika taasisi za afya umelenga zaidi kujali afya za wagonjwa na kuwataka kuwa na utaratibu endelevu katika kuunga mkono jitihada za serikali.

"Kwa niaba ya uongozi napongeza uamuzi huu na siku nyingine msisite kuja kufanya jambo lolote lenye tija katika sekta ya afya, lakini pia tunakaribisha makundi mengine yanayoguswa na mazingira yetu," alisema Dk. Glory.

# Wenye taaluma ujenzi vyoo bora waitwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani, imewataka vijana wa waliopata mafunzo ya ujasiriamali na ujenzi wa vyoo bora kupitia mradi wa ushirikishwaji wa vijana katika ujenzi wa vyoo bora kibiashara (YESB), kuwa chachu ya mabadiliko kwenye jamii.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, wakati wa kufunga mafunzo ya mradi unaotekelezwa na Shirika la Catholic Relief Service (CRS) na kushirikisha vijana 39 wa kata tatu za wilaya hiyo ambazo ni Sangambi, Chalangwa na Mbugani.

Aliwataka vijana hao kutumia elimu na ujuzi walioupata kuhamasisha jamii ya wananchi wa kujenga vyoo bora na kuvitumia ili kuepuka kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

"Kwenye ziara ambazo tumeanza za kuhamasisha ujenzi wa vyoo tumebaini familia nyingi hazina huduma hiyo, sasa ninyi mmepata mafunzo na mmejua umuhimu wa kuwa na vyoo, nendeni mkasaidie familia zenu kujenga na kutoa hamasa," alisema Mahundi.

Alilipongeza CRS na wadau wengine wanaoshirikiana nao kwa kuanzisha mafunzo hayo ambayo alidai kuwa yatawasaidia vijana walioshiriki kupata ajira pamoja na kusaidia kutoa kuyaweka mzingira safi.

Ofisa wa Mradi wa YESB, Musa Mayage, alisema lengo la mradi huo ni kuwapatia ajira vijana hao ambao wengi wao wanatoka katika familia za kipato cha chini pamoja na kuisaidia jamii kujua umuhimu wa vyoo.

Alisema wakati wanaanza walitoa matangazo kwa ajili ya vijana hao kujitokeza na kwamba walijitokeza vijana 72 kutoka katika kata hizo tatu za Sangambi, Chalangwa na Mbugani, ambapo baada ya usaili walipungua na kubakia 45 lakini walioendelea wakawa 39.

Mayenga alisema vijana hao walipelekwa katika Chuo cha Ufundi Stadi (Veta) cha Mbeya, ambapo walisomea masuala ya ujenzi wa vyoo hivyo kwa muda wa siku 21 kabla ya kurudi tena Chunya kwa ajili ya mafunzo ya ujasiriamali ya siku 10.

Alisema pia taasisi hiyo inashirikiana na taasisi zingine ikiwamo Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (Sido) ambalo linawaandalia vijana hao vifaa, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must) ambacho kinatoa ushauri wa kitaalamu.

Aidha, vijana hao waliiomba Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuvipatia vikundi vyao mikopo ya asilimia nne ambayo huwa inatengwa kwa ajili ya kuwakopesha vijana kutokana na mapato ya ndani.

Akisoma risala ya vijana hao, Spora Edger, ambaye anatoka katika Kata ya Chalangwa, alisema wanakusudia kuandaa andiko la biashara ambalo wataliwasilisha katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kuomba uungwaji mkono.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, aliwahakikishia vijana hao kuwa vikundi vyao vitapewa kipaumbele wakati wa utoaji wa mikopo kwenye vikundi vya wajasiriamali.

Aliwashauri vijana hao kuendelea kusambaza teknolojia waliyoipata kwenye kata zingine ambazo hazipo kwenye mradi ili kuwezesha wilaya nzima kuwa na teknolojia hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (mwenye suti), akiwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilomba mwishoni mwa wiki, akiangalia eneo la barabara ya Ilomba ambayo ilikuwa imeharibika vibaya kutokana na mvua zilizonyesha kabla ya Tarura kuifanyia marekebisho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waomba kushirikishwa migogoro na hifadhi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wilayani Mbarali wameiomba serikali iwashirikishe katika kila hatua ya uwekaji wa mipaka baina yao na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wakati wa utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kumaliza migogoro.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati jopo la mawaziri nane wakiongozwa na mwenyekiti wao, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, lilipofika kusikiliza maoni ya wananchi hao ili kumshauri vizuri Rais.

Waliwaeleza mawaziri hao kuwa wakati wa kuweka mipaka ambayo imekuwa ikileta migogoro hawakuwahi kushirikishwa hali iliyosababisha maeneo ya wananchi kumegwa.

Christopher Uhagire, mkulima, alisema awali wananchi hao walishirikishwa lakini wataalamu walipoenda kuandaa tangazo la Serikali la mwaka 2008 walibadili mipaka ya waliyokubaliana na wananchi.

Alisema hali hiyo ilisababisha mgogoro kutokana na wananchi wa vijiji 33 kutakiwa kuondoka katika maeneo yao tofauti kabisa na mipaka waliyokuwa wamekubaliana awali.

"Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kuwa zoezi hili lifanyike kwa uwazi na uwazi huo ni kwamba mipaka watakayoridhia wananchi ndiyo iingie kwenye sheria ili kumaliza kabisa migogoro ya mipaka hii na tunaomba tushirikishwe katika kila hatua ili tuwe na majina ya maeneo zitakapowekwa alama," alisema Uhagire.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama cha wafugaji Wilaya ya Mbarali, Makresia Pawa, alisema Tangazo la Serikali la Mwaka 2008 (GN. 28) limewatesa wakulima na wafugaji wa wilaya hiyo kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Alisema kutokana na hali hiyo, baada ya Rais kutangaza zaidi ya vijiji na vitongoji nchini vinavyodaiwa kuwa viko kwenye hifadhi visiondolewe, wao walikuwa wa kwanza kumshukuru kutokana na tangazo hilo kuanza kuleta nafuu kwao.

Alisema kwa sasa wako tayari kutoa ushirikiano kwa wizara zote zinazohusika katika zoezi hilo la uwekaji wa mipaka na kwamba wako tayari kuiheshimu mipaka hiyo na kuilinda kwa manufaa ya taifa.


"Sisi kwa sasa tumefurahi na tupo tayari kutoa ushirikiano kwa serikali yetu, tutasaidia utoaji wa takwimu na taarifa sahihi kwa Waziri wa Mifugo pamoja na Waziri wa Ardhi, ili taarifa hizo zisaidie kuboresha mazingira," alisema Pawa.

Mbunge wa Mbarali, Haroon Premohamed, alimshukuru Rais Magufuli kwa uamuzi wake wa kusitisha uondoaji wa vijiji 33 vya wilaya hiyo, ambavyo vilikuwa vinadaiwa kuwa ndani ya hifadhi kwa madai kuwa uamuzi huo umezingatia zaidi maslahi ya wananchi.

Alisema wakulima na wafugaji wa wilaya hiyo wataanza kufanya kazi zao kwa uhuru baada ya utekelezaji wa agizo hilo na kwamba ujio wa mawaziri hao ni ishara tosha kuwa sasa utekelezaji umeanza.

Lukuvi alikiri kuwa wananchi hao hawakushirikishwa katika zoezi la awali na kwamba sasa wao wameanza rasmi kuwashirikisha baada ya maagizo ya Rais Magufuli.

Aliwataka waendelee kuwa wavumilivu wakati serikali ikiendelea kulishughulikia suala hilo, huku akiwahakikishia wananchi hao kuwa agizo la Rais liko pale pale na ni lazima watalitekeleza haraka iwezekanavyo.





## UWT yalaani mauaji watoto mkoani Njombe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), imelaani mauaji ya watoto yaliyotokea hivi karibuni mkoani Njombe, na kuvitaka vyombo vya sheria kuwachukulia hatua kali wote waliohusika.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Queen Mlozi, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumuza na wajumbe wa jumuiya hiyo katika maadhimisho ya miaka 42 ya kuzaliwa kwa CCM.

Alisema UWT inalaani mauaji ya watoto ambayo yamekuwa yakifanyika mkoani Njombe, hivyo ni vyema vyombo vya dola vikahakikisha vinatimiza wajibu wake katika jambo hilo.

"Niwaombe waheshimiwa mahakimu kwa wale wote ambao wamebainika kushiriki katika namna moja au nyingine sheria ichukue mkondo wake ili iwe fundisho kwa wangine," alisema Mlozi.

Aidha, aliwataka wanawake kuendelea kushikamana katika kuhakikisha kuwa wanatoa taarifa za mauaji hayo ya kikatili ambayo yamekuwa yakifanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

"Mauaji haya ya kinyama katika taifa letu tunatakiwa kupaza sauti zetu sisi kama wanawake kupigia kelele vitendo hivi vya mauaji ya watoto," alisema.

Aidha, jumuiya hiyo ilimpongeza Rais John Magufuli kwa jitihada zake ambazo ameendelea kuzionyesha za kuwaamini wanawake katika nafasi mbalimbali za kitaifa.

"Hivi karibu wakati Rais akitangaza uteuzi wa majina ya majaji aliweza kuwapatia nafasi majaji wanawake watano, kwa hali hii sisi kama Jumuiya tunampongeza sana na tunaahidi wanawake hatutamwangusha," alisema.

Katika kuadhimisha miaka 42 ya kuzaliwa kwa CCM, pia jumuiya hiyo ilifanya shughuli mbalimbali za kijamii, ikiwamo kuwatembelea wafungwa wanawake katika Gereza la Isanga na kuwapatia vifaa mbalimali, ikiwamo sabuni na mafuta.

Pia walitembelea wodi ya kinamama katika hospitali ya mkoa pamoja na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato na kutoa msaada wa sabuni, kalamu na madaftari.

# Kalemani ataka REA mpya iache migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amezindua bodi mpya ya Wakala wa Umeme Vijijini(REA), huku akiagiza kuacha migogoro itakayokwamisha utendaji kazi wa wakala huo.

Dk. Kalemani alizindua bodi hiyo jana baada ya kuvunjwa Novemba mwaka jana, kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushindwa kutekelezavyema majukumu yake.

Akizungumza na wajumbe wa bodi hiyo, waziri huyo alisema awali ilijitokeza migogoro katika wakala huo hali iliyosababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Pamoja na agizo hilo, Dk. Kalemani aliitaka kusimamia majukumu ya REA kwa mujibu wa sheria ili itekeleze majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha yaliyojitokeza katika bodi iliyopita yasijitokeze tena.

"Migogoro katika sehemu za kazi ni chanzo cha kutokamilisha lengo la kufikisha huduma ya umeme katika maeneo ya vijiji na vitongoji," alisema.

Alisema kuwa migogoro mingine ambayo imekuwa ikitokea inasababishwa na watumishi na bodi yenyewe, hivyo miradi kushindwa kukamilika kwa wakati. "Kwa mara nyingine tena leo nina kazi ya kuzindua bodi mpya na kuikabidhi majukumu yake, tufanye kazi ya kuhakikisha huduma ya umeme inafika huko vijijini na vitongojini hadi ifikapo mwezi Juni mwaka huu awamu ya tatu raundi ya kwanza iwe imekamilika, na tuwasimamie vyema makandarasi wanaosimamia miradi kwenye maeneo mbalimbali," alisema Dk. Kalemani.

Alisema kuwa miradi hiyo itakapokamilika mapema itawezesha kuanza awamu nyingine ili kufikia lengo la serikali la kuhakikisha kuwa maeneo yote ya vijijini na vitongoji yanapata umeme ifikapo mwaka 2021.

"Kulikuwa na migogoro isiyoisha na mingi inasababishwa aidha na wafanyakazi wenyewe ama na bodi wenyewe kwa hiyo kama bodi ni vyema muepuke kabisa migogoro," aliagiza Waziri Kalemani.

Alisema kuwa makandarasi wengi kwa sasa hawafanyi kazi zao kama inavyotakiwa kwa sababu bodi ilikuwa imezorota, hivyo ni matumaini yake kuwa wataenda kusimamia ili kazi zao ziende kwa kasi na kwa ufanisi zaidi.

Waziri huyo alisisitiza bodi hiyo inayoongozwa na Mwenyekiti, Michael Nyagoga, kusimamia sheria ili kuhakikisha kuwa maeneo yote yanafikiwa na umeme na kukamilisha azma ya serikali ya uchumi wa viwanda.



Mkuu wa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, Simon Odunga (kulia), akisoma moja ya bango lilionyeshwa na wananchi wa Kijiji cha Lahoda wilayani humo, kuhusu malalamiko dhidi ya viongozi wa kijiji na diwani kuuza maeneo ya kijiji yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wachimbaji wadogo Chamwino kukaguliwa


**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

MWENYEKITI wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, ameagiza Ofisi ya Madini Dodoma kuitisha kikao cha wachimbaji wadogo wadogo kitakachokagua kumbukumbu za uzalishaji wao, ulipaji wa maduhuli na ushiriki wao katika huduma za kijamii.

Prof. Kikula alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika kijiji cha Kwahemu wilayani Chamwino na kubaini kuwapo na idadi kubwa ya wachimbaji hao wa madini aina ya nikel milimani.

"Ofisa madini hakikisha mnaitisha kikao msikilize kero na madukuduku yao, pia waje na records zao za production na ulipaji maduhuli na wameshiriki vipi kwenye huduma za kijamii, wote waje na kumbukumbu hizi," alisema. Kwa upande wake, Ofisa Madini Mkoa, Jonas Mwano, aliahidi kuitisha kikao haraka iwezekanavyo, huku akisema kuwa awali waliitisha kikao na wawekezaji wote waliulizwa wamefanya nini kwenye mrabaha wa serikali, huduma kwa jamii na tozo ya huduma.

"Tuliwapa elimu ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 kuhusu wanachotakiwa kutoa kwa serikali na jamii inayowazunguka na Mkuu wa Mkoa alitoa maazimio mikataba iingiwe kwa kipindi cha mwaka mmoja, mwekezaji afike kwenye kijiji husika na achukue kitu anachotakiwa kufanya,"alisema.





Wachuuzi wa dagaa katika soko la samaki la Kibirizi kwenye Manispaa ya Kigoma Ujiji, wakianika dagaa sokoni hapo. **PICHA: OWM**

# Oman yajivunia uwekezaji Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Kampuni ya Arabian Industries ya Oman, Sheikh Amor Al -Suleimani, amesema Oman inajivunia kuona wawekezaji wa taasisi na kampuni za kibiashara kutoka nchi hiyo, wanashawishika kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye miradi ya utalii na uvuvi wa Bahari Kuu.

Amesema anaamini uwekezaji huo utaongeza mapato na kuimarisha uchumi wa nchi hizo mbili.

Aliyasema hayo Chukwani mwishoni mwa wiki alipozungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi.

Al – Suleimani alimweleza Balozi Iddi kuwa, wananchi wa Zanzibar na Oman hawana sababu ya kutoshirikiana kutokana na uhusiano wao wa kihistoria. Alisema uongozi wa Arabian Industries tayari umeshawishika kuwekeza katika miradi ya sekta ya utalii kwa kujenga hoteli ya nyota tano kutokana na fursa za uwekezaji zilizoko visiwani Zanzibar.

Akitoa shukrani zake kwa ujio wa ujumbe huo wa Arabian Industries, Balozi Iddi alisema Zanzibar imezungukwa na samaki kutokana na kuwa na bahari pembe zake zote inayotoa fursa kwa wawekezaji wa nje kuanzisha miradi yao ya uvuvi wa Bahari Kuu.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (Zipa) iko tayari kushirikiana na taasisi au kampuni itayojitokeza kuwekeza kwenye sekta hiyo yenye uwezo wa kutoa ajira nyingi kwa wazawa ili kupunguza ukali wa maisha.

Balozi Iddi pia alikutana kwa mazungumzo na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, aliyefika Zanzibar kujitambulisha rasmi baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo.

Dk. Damas Ndumbaro alisema anatambua umuhimu wa Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo bado ana safari ndefu ya kujifunza mambo mengi kutoka kwa watangulizi wake.

# 'Mapinduzi yameimarisha elimu'

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, amesema ustawi wa elimu nchini umetokana na matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika hafla ya kuwapatia zawadi wanafunzi waliofaulu kwa kupata alama za daraja la kwanza na la pii katika mtihani wa kidato cha nne mwaka jana kutoka shule mbalimbali za Zanzibar, iliyofanyika kwenye viwanja vya Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Unguja.

Dk. Mabodi alisema baada ya kufanyika Mapinduzi ya Zanzibar, serikali ya wakati huo ilitangaza kuwa, suala la elimu ni bure huku ikiimarisha miundombinu ya upatikanaji wa elimu kwa wananchi wote bila ubaguzi.

Alisema CCM itaendelea kuenzi tunu ya mapinduzi kutokana na mambo mema yaliyotekelezwa kwa haraka mara tu baada ya kufanyika kwake na wananchi wakapata uhuru na kunufaika na fursa ya elimu iliyotolewa kwa ubaguzi kabla ya mapinduzi hayo.

Alisema kwa sasa, Zanzibar imekuwa ni kitovu cha wasomi na watu wenye taaluma mbalimbali ambao chanzo cha mafanikio hayo kimetokana na kukua kwa sekta ya elimu nchini. Dk. Mabodi pia aliwapongeza wanafunzi waliofaulu vizuri katika mtihani huo na kuwashauri waliofeli kutokata tamaa, wajiendeleze kupitia sekta ya mafunzo ya amali ili wawe na ujuzi. Alisema katika kuunga mkono elimu, CCM imeandaa mpango maalum wa kuwasaidia vijana waliofeli masomo yao, katika ngazi tofauti za kielimu ili nao wapate ujuzi wa kujiajiri wenyewe.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohamed Mahmoud, aliwataka wanafunzi waliofaulu mtihani huo, kusoma kwa bidii ili wafaulu vizuri mtihani wa kidato cha sita na kujiunga na vyuo vikuu.

Alisema elimu ni jambo muhimu kwa maisha ya binadamu, hivyo ni lazima wajitume katika safari yao ya kutafuta taaluma.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Unguja, Angelina Adam Malembeka, aliwaambia wanafunzi hao kuwa, bado wana safari ndefu ya kutafuta elimu, hivyo waendelee kusoma kwa bidii ili wafikie malengo yao.

Wanafunzi 1,222 waliofaulu mtihani wa kidato cha nne kwa kiwango cha daraja la kwanza na la pili, walipatiwa zawadi mbalimbali na CCM.

## Serikali yaipongeza sekta binafsi kuimarisha elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inathamini mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi kukuza na kuimarisha maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Akizungumza katika mahafali ya 10 ya Shule ya Phelter Federal iliyoko Fuoni Wilaya ya Magharibi 'B', Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmod, alisema mchango unaotolewa na shule za watu binafsi unasaidia kuchochea kasi ya maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Alisema kutokana na mabadiliko ya kisera na sheria mwaka 1990, Serikali ya Zanzibar ilitoa fursa kwa sekta binafsi kuanzisha shule ili kufikia malengo ya kupanua miundombinu na kuimarisha ubora wa elimu kwa wananchi wake.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kulipa ada za watoto wao kwa wakati ili kuuwezesha uongozi wa shule hiyo kutekeleza vyema majukumu yake.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliwataka wahitimu na wanafunzi kwa ujumla kutumia kikamilifu uwapo wa fursa ya elimu bila malipo, kutafuta elimu na ujuzi utakaoimarisha utaalamu katika nyanja mbalimbali.

Alisema serikali ya mkoa wake itaendelea kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu kwa shule zote za serikali na binafsi bila ya ubaguzi ili mkoa huo uendelee kupaa kielimu.

Awali, katika risala yake, uongozi wa shule hiyo ulisema kuwa pamoja na kupata mafanikio makubwa ya ufaulu, shule hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa vifaa vya maabara, madawati na kuchelewa kwa wazazi kulipa ada za watoto wao.

Katika mahafali hayo, Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe ambaye pia ni Naibu Waziri wa Sheria, Katiba na Utawala Bora, Khamis Juma Mwalim, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuendelea kuwasimamia vyema watoto wao na kuachana na tabia ya kuwaozesha vijana wakiwa skuli ili kuwajengea mazingira bora ya maisha yao ya baadaye.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 Feb**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Delirious
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 24 Feb**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt - Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Green Light 2
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Kisasi cha utata
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## EATV




EATV

# LEO USIKU SAA 3:00



**JUMATATU**
11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:00 UTAKE
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 KURASA
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 UJENZI
21:30 5SPORTS LIVE
22:30 BONGO HITS

***Ujenzi** Fahamu mambo mbalimbali kuhusu ujenzi, mapambo ya nyumba nje na ndani, mitindo na teknolojia tofauti zitumikazo kwenye ujenzi.*

## eastafrica RADIO

05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11.00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

**CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM**
**FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE**

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## Trump ayataka mataifa Ulaya kuwapokea ISIS

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameyataka mataifa ya Ulaya kuwachukua mamia ya wapiganaji wa kundi la Dola la Kiislamu nchini Syria.

"Marekani inazitaka Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na mataifa mengine washirika wa Ulaya kuwachukua zaidi ya wapiganaji 800 ambao wamekamatwa nchini Syria na kuwafikisha mahakamani," alisema Rais Trump kwenye akaunti yake ya Twitter na kuongeza.

"Marekani haitaki kuwa walinzi wa wapiganaji hawa wa ISIS kutoka Ulaya, ambako ndiko wanatarajiwa kwenda.

"Tunafanya mengi na tunatumia fedha nyingi, sasa wakati umefika kwa wengine kuchukua jukumu hilo na kufanya kazi ambao wanaweza sana kuifanya. Tunaondoa majeshi yetu baada ya ushindi wa asilimia 100."

Ujumbe huo katika Twitter umekuja baada ya Makamu wa Rais Mike Pence kutoa wito kwa mataifa mengine kuchukua jukumu nchini Syria wakati vikosi vya Jeshi la Marekani vikiondolewa.

Akiwa katika mkutano wa usalama mjini Munich, Rais Trump, aliwaambia waandishi wa habari kwamba Marekani inataka mataifa mengine kutoa vikosi vya jeshi na mengine vifaa kusaidia kuilinda Syria.

*DW*

## Miili 24 yaopolewa kwenye migodi Zimbabwe

**HARARE, Zimbabwe**

WAOKOAJI nchini Zimbabwe wameiopoa miili 24 ya watu waliokufa kwenye migodi miwili ya dhahabu iliyokumbwa na mafuriko juzi, ambapo watu wanane wameokolewa.

Kwa mujibu wa televisheni ya taifa ya nchini Zimbabwe, kuna hofu kwamba wachimbaji kadhaa walio nchini humo kinyume cha sheria bado wamekwama ndani ya migodi hiyo.

Shughuli za uokoaji bado zinaendelea katika migodi hiyo ambayo ilikuwa karibu na mji wa Kadona ulipo kilomita 145 kusini magharibi mwa mji mkuu Harare.

Mnamo siku ya Ijumaa serikali ilitangaza juu ya kukwama kwenye migodi hiyo miwili wachimbaji wapatao 70.

*DW*

# Tume ya uchaguzi Nigeria yakanusha kushawishiwa kisiasa

**LAGOS, Nigeria**

WAKATI wagombea uchaguzi nchini Nigeria wakishutumiana kwa tangazo la ghafla la kuahirishwa uchaguzi, tume ya uchaguzi imesema tangazo hilo halikushinikizwa kisiasa wala kiusalama.

Wagombea wakuu wa uchaguzi nchini humo wamekuwa wakitupiana lawama kutokana na uamuzi wa ghafla uliochukuliwa na tume ya uchaguzi kuahirisha uchaguzi wa rais kwa wiki moja hadi Februari 23, kila mmoja akimnyooshea kidole cha lawama mwenzake.

Uamuzi wa kuahirisha uchaguzi uliotangazwa saa tano kabla ya vituo vya kupiga kura kufunguliwa siku ya Jumamosi.

Uchaguzi huo unatarajiwa kugharimu nchi hiyo dola bilioni 2 za Kimarekani, sambamba na kuiathiri hadhi ya taifa hilo kubwa kabisa kufuata mfumo wa kidemokrasia barani Afrika.

Kwa sasa, mamlaka zinazohusika na uchaguzi nchini Nigeria zina kazi ya kuamua namna ya kuvifanya vifaa vya kupigia kura ambavyo tayari vilishawasilishwa kwenye vituo vya kupigia kura, huku hali ikiwa ya wasiwasi kutokana na matukio ya hivi karibuni wakati majengo ya tume ya uchaguzi yakichomwa moto.

Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi, Mahmood Yakub, aliwaambia waangalizi, wanadiplomasia na waandishi wa habari kwamba kucheleweshwa kwa uchaguzi hakuhusiani na hali ya ukosefu wa usalama wala kuingiliwa kati kisiasa.

"Mazingira mabaya ikiwamo hali mbaya ya hewa ndiyo iliyosababisha kuchelewa kwa ndege zilizobeba vifaa na pia moto kwenye ofisi tatu za tume, Ni muhimu sana kwa wananchi kuupokea uchaguzi ulio huru, wa haki na wenye kuaminika," alisema Yakub.

Alisema hadi kufikia majira ya saa nane usiku walikuwa na uhakika kwamba uchaguzi ungelifanyika, huku akihakikisha kuwa tarehe 23 Februari haina mjadala tena.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa nchini Nigeria wanasema ikiwa uchaguzi ungelikwenda kama ulivyokuwa umepangwa, vituo vya kura visingeliweza kufunguliwa kwa wakati mmoja nchi nzima.

Wapigakura wenye hasira katika mji mkuu, Abuja, ambao walitoka majumbani kwao kwenda kupiga kura zao, wakiwamo raia wengi wa nchi hiyo wanaoishi mataifa ya nje, walisema wasingeliweza tena kubakia kwa siku saba nyingine na kuonya kwamba huenda watu wakagomea kupiga kura.

Wengine walionyesha hasira zao kutokana na kulazimika kupanga upya shughuli zao ikiwamo mitihani na harusi.

DW



Afisa wa polisi akilinda doria wakati wafanyakazi wa tume ya uchaguzi Nigeria wakipakia vifaa vya kupiga kura katika malori ili kuvipeleka katika vituo vya kupiga kura eneo la Yola, Nigeria.**PICHA: VOA**

# Mbunge ajiuzulu baada ya kuiba mkate

**LYUBLYANA, Slovenia**

MBUNGE mmoja nchini Slovenia, Darij Krajcic, amejiuzulu baada ya kuiba mkate maarufu "sandwich" katika duka moja kwa madai kuwa wahudumu wa sehemu hiyo walimpuuzia.

Krajcic aliviambia vyombo vya habari vya ndani kuwa alipuuzwa na wafanyakazi wa duka hilo na walikuwa wakiendelea na shughuli zao wakati yeye akihitaji huduma.

Hakubainika kama ameiba lakini baadaye baadhi ya wanachama walisisitiza arudi kulipa pesa ya mkate huo.

Hata hivyo, Krajcic aliomba msamaha na kusema kuwa anajutia kitendo alichokifanya.

Suala lake la kuiba lilisambaa baada ya kuwaambia wabunge wengine wakati wa mkutano wa kamati.

"Nilisimama pale kwa dakika tatu, kabla wanihudumie," mbunge huyo mwenye miaka 54 alisimulia katika kituo cha runinga.

Alisema wafanyakazi watatu wa duka hilo hawakugundua kama yupo ambapo walikuwa na mazungumzo baina yao hali iliyosababisha profesa huyo wa zamani kujaribu bahati yake.

Alisema hakuna mtu yeyote aliyepiga kelele, wala kumfuata, wabunge wenzake walicheka baada ya kusikia kisa hicho.

Lakini siku ya Alhamisi Spika wa Bunge hilo, Brane Golubovic, alikemea vikali kitendo cha mbunge kuiba na kusema kuwa ni kitendo kisichokubalika.

Akizungumza na vyombo vya habari, Golubovic alisema Krajcic amechukua hatua za kuwajibika na kujiuzulu yeye mwenyewe.

*BBC*

# DRC yakoshwa na Tasaf kwa upunguzaji umaskini

**Na Elizabeth Zaya, KIBAHA**

MAOFISA wa Mfuko wa Huduma za Jamii kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), wamepongeza Tanzania kwa kufanya vizuri katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia miradi yake ya uhawilishaji fedha kwa kaya maskini zimeanza kuwa na uhakika wa kujikimu kimaisha.

Akizungumza katika ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu iliyofanywa na Maofisa hao Kibaha mkoani Pwani, Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo( FSRDC), Ruphin Bo_Elongo, alisema, Tanzania imepiga hatua katika mpango huo tofauti na ilivyo kwa nchi yao.

"Tanzania wako mbali sana katika uwezeshaji wa kaya maskini, ni nchi ambayo haipaswi kubezwa kwa hatua hizi walizopiga katika kupunguza umasikini na ndio maana tumeamua kuja kujifunza kutoka kwao na tunaamini tukirudi kwetu tutafanya uboreshaji mkubwa na sisi kutokana na haya tuliyojifunza kutoka TASAF Tanzania," alisema Elongo.

Alisema utaratibu wote unaoendeshwa na TASAF Tanzania, katika ncho yao haupo na kwamba watahakikisha wanafuata mbinu zote walizojifunza ili kusaidia kaya masiki nchini mwao.

Akitoa taarifa mbele ya Maofisa hao, Mratibu wa TASAF kwa mkoa wa Pwani, Asha Itewele, alisema kuanzia Januari 2014 hadi Desemba 2018 Mkoa ulipokea jumla ya Sh. bilioni 29.89 kwa ajili ya kusaidia kaya hizo.

Alisema kupitia mpango huo kaya maskini zimeanza kuwa na uhakika wa kujikimu kimaisha na kujifunza namna ya kujiwekea akiba.

Alisema pamoja na faida ambazo walengwa wamezipata, lakini pia kwa sasa zaidi ya asilimia 85 ya walengwa wanapata huduma za afya huku kukiwa na ongezeko la kaya hizo kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), kuendesha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato na watoto kuhudhuria vizuri shuleni.

Akizungumzia kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Mratibu wa TASAF wa halmashauri hiyo, Sijaona Muhunzi, alisema, mpango huo umesaidia kuongeza idadi ya mahudhurio shuleni kwa kiwango kikubwa kwa watoto wa walengwa.

"Kwa sasa mahudhurio ya watoto shuleni yako juu, wana uhakika wa chakula na mavazi ya shule, lakini wazazi wao wamehamasika sana kwa kusimamia maendeleo ya watoto wao, tulianza kutoka sifuri katika kuhamasisha watoto wa kaya masikini kwenda shule lakini mpaka sasa watoto wanahudhuria kwa asilimia 98.68 tangu kuanza kwa mpango hadi kufikia Desemba mwaka jana," alisema Muhunzi.

Mmoja wa wanufaika, Halima Kibavu, mkazi wa Kijiji cha Vikuge Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, aliipongeza serikali kutokana na mpango huo kumnusuru umaskini aliyokuwa nao.

Alisema msaada anaopewa na kwa Maofisa wa Mfuko huo, vimemsaidia kuanzisha miradi ya ufugaji na kilimo ambacho kimemsaidia kuondokana na umasikini.



Dereva wa bodaboda, Samuel Gasper Kisanga, akizungumzia ubora wa mafuta ya Total, yenye kiambata cha Excellium, mwishoni mwa wiki kampuni hiyo ilipotoa punguzo la shilingi 70 katika bei ya mafuta yake kama ishara ya upendo kwa Watanzania katika kusherehekea Sikukuu ya Wapendanao (Valentine). **MPIGAPUCHA WETU.**

# RC Hapi ashtukia waganga wa jadi

**Na George Tarimo, IRINGA**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amepiga marufuku utoaji wa maombi yote au vibali vya utoaji wa leseni kwa waganga wa jadi mkoani hapa.

Hapi amesema lengo la kufanya hivyo ni kubaini wingi wa waganga wanaowadanganya wananchi kwa lengo la kijipatia fedha haramu sanjari na imani za kishirikina.

Uamuzi huo umetokana na kupokea ripoti ya ukatili wa kingono kwa watoto kutoka kwa watafiti wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE).

Utafiti huo umefanywa na jopo la watafiti wakiongozwa na mhadhiri wa MUCE, Nicodemas Matojo, ambao walibaini kuwa Mkoa wa Iringa una waganga wa jadi zaidi ya 800 waliosajiliwa na wengine zaidi ya 700 ambao hawatambuliwi.

Hapi alisema hayo kwenye mkutano maalumu wa kamati ya ushauri ya mkoa (RCC) na kusema akiwa kama kiongozi mkuu wa mkoa huo, ameamua kusitisha huduma hiyo ya kada ya waganga wa kienyeji ili kuchunguza shughuli wanazozifanya na jinsi walivyopata leseni za kutoa huduma hiyo.

Alisema waganga wengi wa jadi wakishirikiana na watendaji wa vijiji wanapewa rushwa kwa lengo la kuzungumza na viongozi wa juu wa wilaya au mkoa ili nyaraka zao zinapofika ziweze kupita na ndio maana wanapata waganga wengi ambao hawana maadili ya uganga ma kufanya shughuli zao kinyume cha taratibu za nchi zinavyoelekeza.

Alisema serikali inapambana kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za rufani nchi nzima ili wananchi waweze kupata matibabu, lakini kumekuwa na ongezeko la waganga wa kienyeji wadanganyifu ambao wanawarubuni wananchi kutibiwa kwao badala ya kutibiwa hospitali zinazotambulika na ndio maana vitendo vya ukatili haviishi.

Hapi alivitaka vyombo vya dola ikiwamo Jeshi la Polisi na vyombo vingine kushirikiana na ofisi ya mganga mkuu wa mkoa kuchambua kwa kina waganga wenye leseni zaidi ya 800 ili kutambua walipataje leseni zao.

# Wahamiaji haramu wafungwa miaka sita

**Na George Tarimo, IRINGA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Iringa, imewahukumu kifungo cha miezi sita kila mmoja wahamiaji haramu kwa kosa la kuingia nchini bila vibali.

Aidha, wahamiaji wengine saba raia wa Ethiopia na mmoja wa Zambia kesi yao iliahirishwa baada ya kukosekana mkalimani wa lugha wanazozungumza.

Akiwasomea mashtaka mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Iringa, Liadi Chamshama, mwendesha mashtaka wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Iringa, Lameck Chiloli, alidai mshtakiwa wa kesi namba 10 ya mwaka 2019, Samuel Kamani (25) raia wa Kenya, alikamatwa katika kituo cha mabasi mjini Iringa na kushtakiwa kwa kosa la kuwapo nchini bila kuwa na paspoti wala kibali chochote kinachomruhusu kufanya hivyo.

Mshtakiwa mwingine katika kesi namba 8 ya mwaka 2019, John Kailanga (27), raia wa Uganda, aliyekamatwa Januari 20, mwaka huu akiwa nchini bila kibali kinyume cha sheria namba 45 kifungu cha kwanza (i) na cha pili chini ya marekebisho ya mwaka 2016.

Katika kesi nyingine namba 9 ya mwaka 2019 raia wa Zambia, Jon Bwalya, kesi yake imeahirishwa kutokana na kukosa mkalimani wa lugha ya Kibemba sambamba na raia wengine wa Ethiopia ambao kesi yao namba 5 ya mwaka 2019 ambao nao kesi yao imeahirishwa hadi Februari 21, mwaka huu baada ya kukosa mkalimani. Kamanda wa Uhamiaji mkoani Iringa, Tununasia Adam, alisema watuhumiwa walikamatwa katika operesheni ya kusaka wahamiaji haramu iliyofanyika kati ya Desemba mwaka jana na Januari mwaka huu.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

**ENEO LINAUZWA,** Nauza eneo liko mpiji magoe yanapogeukia magari ya kutoka mbezi ni unatembea mita mita mia miambili hadi kwenye eneo ukubwa ni mita 20@40 bei nafuu kabisa simu no 0621607825

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

## MAGARI

**MAGARI YANAUZWA,**

1.LEYLAND DAF TANI 4, DIESEL, SAFI SANA, 4200 CC.

2.LEYLAND DAF TANKI YA MAJI LITA 8000 DIESEL 5800 CC. KUBADILISHANA NA GARI NYINGINE, PIGA SIMU NAMBA 0657 370655.

*Uza Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

Yetu Microfinance Bank PLC

**Wekeza nasi katika akaunti maalum upate faida kubwa.**

**Muda wa uwekezaji:** Miaka miwili

Kwa mwekezaji mwenye kiasi cha zaidi ya million 50, tafadhali piga simu 0762623062

**Unaweza kuwekeza kuanzia shilingi million moja kwa faida ya hadi 13%**

215048502

**NYUMBA INAUZWA TABATA**

NYUMBA INAUZWA ILIYOPO TABATA CHANG'OMBE YENYE VYUMBA 3 IKIWEMO MASTER MOJA, PUBLIC TOILETS, STORE, DINNING, JIKO, PARKING YA MAGARI (BEI NAFUU).

**MAWASILIANO:** 0786 058343 / 0654 969280 / 0622 096682.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya Mwanzo CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**MADAIWA NAMBARI 377/2018**
**Mdai: LISIOUSLIGHT FINANCIAL LTD.**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: MICHAEL LUBOTE NHONYA**

Kwa : MICHAEL LUBOTE NHONYA

KWA kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba Madai ya Tsh. 3,554,000/=

Kwahiyo Unahitajika/Mnahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya alhamisi tarehe 28/02/2019 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashaidi wako/wenu na hati zote zilizohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurirni hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshidwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14/02/2019.

215066802

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la The Guardian kila siku*

*Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO? Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# Griezmann, Costa, Morata kuanza pamoja Atletico

**MADRID, Hispania**

KURUDI kwa Diego Costa kutoka chumba cha majeruhi kunamaanisha kwamba Atletico Madrid wanaweza kumtumia mshambuliaji huyo pamoja na Alvaro Morata na Antoine Griezmann mbele kama washambuliaji watatu, amesema kocha Diego Simeone.

Costa aliingia akitokea benchi baada ya wiki 10 za kuwa nje ya dimba kutokana na majeraha, wakati Atletico ikishinda bao 1-0 dhidi ya Rayo Vallecano na kujivuta kwenye nafasi ya pili kwenye La Liga Jumamosi.

Kuwasili kwa Morata akitokea Chelsea wakati wa dirisha la Januari, kumeimarisha safu ya ushambuliaji ya kocha Simeone, lakini alikuwa ni Greizmann ambaye alifunga bao hilo pekee katika kipindi cha pili.

Mshambuliaji huyo amepanda juu ya Fernando Torres na kuwa nafasi ya tano kwa kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Atletico akifunga mabao 130.

Simeone alimtumia Greizmann na Thomas Lemar kama mawinga wakati Costa alichezeshwa kama mshambuliaji wa kati akiwa patina na Morata, lakini anapanga kuwachezesha washambuliaji wote hao watatu kwa pamoja.

"Napenda, lakini inahitaji muda, kufanya kazi kwa bidii na watacheza wote watatu kwa pamoja," alisema kocha huyo, ambaye amesaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia hapo.

"Nina matumaini kwa nafasi fulani naweza kuwatumia zaidi. Kuingia kwa Lemar kulifanya timu icheza kwa kujiachia."

# Sanchez ahofia kiwango chake



**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez, amebainisha kwamba ana hofu kwa kushindwa kuleta furaha kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England na mashabiki wake.

Sanchez ameshindwa kuwa kwenye kiwango chake tangu alipotua hapo akitokea Arsenal Januari mwaka jana, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, akifunga mabao matano tangu awe mchezaji wa United.

Kocha wa muda wa United, Ole Gunnar Solskjaer amesema hawezi kumsaidia Sanchez baada ya mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona kuonyesha kiwango kibovu katika mchezo waliofungwa 2-0 na Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku akikabiliwa na mchezo wa Kombe la FA leo Jumatatu wa raundi ya tano dhidi ya Chelsea, Sanchez amesema anatakiwa kuonyesha ubora wake hapo katika dimba la Old Trafford.

"Yeye (Solskjaer) hajawahi kuzungumza na mimi nini ninachotakiwa kufanya dimbani, lakini nafikiri mimi ni mchezaji mzoefu na nafikiri najua nini ninachotakiwa kufanya," alisema Sanchez akiiambia BBC.

"Mimi ni mchezaji na sina mkataba na mpira, kuna wakati nataka kucheza kila mchezo. Lakini kuna wakati upo ndani na wakati mwingine upo nje."

# Pique:

## Barca inatakiwa kuimarisha kiwango

**BARCELONA, Hispania**

GERARD Pique ametaka kuimarika zaidi kwa kiwango wakati Barcelona ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga dhidi ya Real Valladolid.

Sare dhidi ya Valencia na Athletic Bilbao na ile dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'], kulionyesha kutokuwa kwenye ubora kwa kikosi hicho cha kocha Ernesto Valverde.

Penalti ya kipindi cha kwanza ya Lionel Messi ilitosha kuwafumua Valladolid, ingawa golikipa Jordi Masip aliokoa kwa ustadi mkubwa penalti ya pili ya mchezaji huyo raia wa Argentina.

Hivyo, ina maanisha kwamba Barcelona watakwenda kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lyon wakiwa wanaongoza kwa pointi sita kileleni mwa msimu wa La Liga baada ya mechi 24, lakini Pique anaona kwamba wanahitaji kuimarika zaidi kwa kiwango chao.

"Hatukucheza vizuri, haukuwa mchezo mzuri," alisema akiiambia Televisheni ya Movistar.

"Habari nzuri ni kwamba tulipata ushindi, tulirudi kwenye kawaida yetu ya ushindi, lakini tunatakiwa kuimarika.

"Kiwango si cha kuvutia zaidi kwa upande wetu, kwa mchezo wa Jumanne tunatakiwa kucheza vizuri zaidi."

## HABARI MICHEZO

# PENALTI

## BADO ZA MESSI BARCELONA - VALVERDE




**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, hana hofu na upigaji wa penalti wa Lionel Messi baada ya nyota huyo kufunga moja na nyingine kukosa wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Real Valladolid mwishoni mwa wiki.

Ulikuwa ni usiku wenye mambo mengi kwa Messi katika dimba la Camp Nou, wakati nahodha huyo wa Barca vinara hao wa La Liga wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 Jumamosi.

Messi ambaye amefunga mabao 30 au zaidi kwa misimu 11 katika mashindano yote kwa Barca angeweza kuipatia timu yake bao la pili, lakini mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or alikosa penalti dakika ya 85 iliyookolewa na Jordi Masip.

"Hapana, Hapana. Kwa uhakika kabisa sina hofu. Nilikuwa na uhakika kwamba angefunga zote," alisema Valverde akijibu swali alipoulizwa kama ana hofu na upigaji penalti wa Messi.

"Leo ndio mpigaji wetu bora. Hangeweza kufunga mabao yote."

Katika mchezo huo, Barca walionekana kuwa bora zaidi kwenye safu ya ulinzi na waliweza kuwazuia vizuri washambuliaji wa Valladolid.

## Allegri aipa Juve bao la ugenini kwa Atletico

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri, anaamini timu yake itapata bao la ugenini wakati itakapocheza kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16-Bora dhidi ya Atletico Jumatano hii.



Vinara wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, watakwenda kwenye dimba la Wanda Metropolitano kucheza mchezo huo wa mtoano kwenye ligi hiyo.

Allegri ana imani Juve itaweza kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo, lakini ana hofu kwamba Atletico wanaweza kufanya lolote, ambapo wamefuzu kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kwa misimu mitano iliyopita.

"Timu iko imara. Utakuwa mchezo wenye changamoto kubwa," alisema mara baada ya timu yake kuibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Frosinone.

"Atletico wanacheza mchezo mzuri hasa wakiwa wanacheza nyumbani. Ni timu yenye matokeo mazuri Ulaya.

"Ni mchezo utakaokuwa wazi, wote sisi na wao tuna nafasi kubwa ya kusonga mbele.

"Kitu cha kwanza ni kuhakikisha tunafunga bao mjini Madrid. Tukifunga bao Madrid itakuwa nafasi nzuri kwa upande wetu."

# Guardiola asifia kiwango cha Silva

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amemsifia David Silva kwa kucheza kama kijana Phil Foden wakati timu hiyo ikibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Newport County kwenye mchezo wa Kombe la FA raundi ya tano.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England walishindwa kutikisa nyavu katika kipindi cha kwanza katika dimba la Rodney Parade na kuonekana kama mchezo ungekuwa mgumu kwa upande wao.

Leroy Sane aliipita beki ya Newport dakika ya 51, wakati mchezaji wa timu ya Taifa ya Vijana ya England, Foden alifunga mara mbili, huku Riyad Mahrez akifunga la nne.

Kiungo huyo mkongwe, Silva, alikuwa mmoja wa nyota wa City ambaye alianza kwenye mchezo huo na kutolewa dakika ya 82 na alisifiwa mno kwa kiwango chake.

"Ngumu kuamini," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kuhusu uwezo wa mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Hispania mwaka 2010.

"Ana umri wa miaka 33, anapambana kama kijana mdogo, hakika kipaji chake ni cha hali ya juu. "David ni mchezaji anayevutia. Alicheza kama vile kijana Phil Foden mwenye umri wa miaka 18."

City sasa imefuzu kwenda robo fainali ya michuano hiyo na inatafuta uwezekano wa kushinda mataji manne msimu huu.

Watacheza na Schalke kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16 Jumatano kabla ya kuwavaa Chelsea kwenye fainali ya Kombe la EFL katika Uwanja wa Wembley siku nne baadaye.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ROBBEN: ANFIELD KUNANITESA SANA

Wakati Bayern ikiifuata Liverpool kesho, Mholanzi huyo aeleza alivyochezea vichapo akiwa...

**MUNICH, Ujerumani**

NYOTA wa Bayern Munich, Arjen Robben, amesema Anfield ni "uwanja mbaya zaidi" kwake kuelekea mechi ya mtoano ya hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool.

Mabingwa hao wa Bundesliga, Bayern watasafiri kuwafuata wanafainali wa msimu uliopita na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool katika mechi ya kwanza ya hatua ya mtoano kesho.

Robben ambaye ataondoka Bayern mwishoni mwa msimu ana kumbukumbu mbaya hapo Anfield wakati akiwa na Chelsea.

Chelsea ilitolewa kwa tofauti ya bao 1-0 na Liverpool katika mechi ya nusu fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya 2004-05, wakati Robben na wachezaji wenzake walipoteza tena kwa mikwaju ya penalti dhidi ya miamba hiyo ya Anfield katika michuano hiyo ya msimu wa 2006-07.

"Nadhani kama utaniuliza [kuhusu] uwanja mbaya kwangu mimi, pengini ni Liverpool," winga huyo wa Kiholanzi mwenye umri wa miaka 35, aliliambia Gazeti la The Guardian. "Mara zote unakuwa na mpinzani wako anayevutia na mara zote kuna anayekuwa mbaya."

Akiangazia nusu fainali mbili alizochapwa na Liverpool Ulaya, Robben aliongeza: "Kwa wakati huo [Liverpool] walikuwa na uwezo wa kuwa timu ya wapiganaji wa kombe hili, pia katika Kombe la FA au Kombe la [Ligi].

"Katika mechi moja ama mbili ukweli waliweza kuishi katika hilo na kuonyesha ubora; si kwa msimu mzima, ambao pengine ni zaidi. Huo ulikuwa ni ubora wao mkubwa zaidi: walikuwa pale wakati huo wanahitaji kuwapo pale.

"Sasa nadhani imebadilika na wamendelea vizuri sana. Kocha amefanya kazi kubwa. Mwaka jana walicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa na kwa sasa wapo kileleni mwa [Ligi Kuu England]. Ni muda mrefu uliopita ambao walitwaa ubingwa wa Ligi Kuu na ni moja ya kitu wanakiota."

## KWA UFUPI

### CHELSEA YAMGEUKIA ICARDI
Chelsea ipo tayari kumsajili straika wa Inter Milan, Muargentina Mauro Icardi, 25, baada ya Real Madrid kupunguza presha za kuhitaji huduma yake. ***(Sun)***

### GUENDOUZI DADO LULU PSG
PSG bado hajapotezea matumaini yake ya kumsajili kiungo wa Arsenal, Matteo Guendouzi, 19. ***(The Daily Express)***

### POGBA AICHUNGULIA TENA JUVE
KIUNGO wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, 26, amehitaji tena uhamisho wa kurejea klabu yake ya zamani ya Juventus kama sehemu ya kubadilishana na Douglas Costa, 28. ***(Tuttosport, via Star)***

### RABIOT AWAZA KUTUA BARCA
KIUNGO wa Paris St-Germain, Mfaransa Adrien Rabiot, 23, anaamini atajiunga na Barcelona majira ya joto. ***(Le Parisien - in French)***

### HAVERTZ KUMRITHI OZIL
Arsenal inahusishwa na kutaka kutoa ofa kwa kiungo wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz, 19, kama Mesut Ozil ataamua kuondoka 'Gunners'. ***(TalkSport)***

### PSG, UNITED KWA FELIX
Manchester United ipo katika mbio moja na Paris St-Germain za kuwania kumsajili kiungo wa Benifica, Joao Felix, 19, ambaye anaweza kuondoka kwa pauni milioni 105. ***(Mirror)***

### OSPINA KUTIMKA NAPOLI
KIPA wa Arsenal, David Ospina, 30, anayeichezea Napoli kwa mkopo, analazimisha kurejea Amerika Kusini, kufuatia nafasi yake katika kikosi cha kwanza kuwa finyu tangu kurejea kwa kipa chaguo la kwanza, Alex Meret. ***(Goal)***

### MANOLAS AZISHIKA UTD, ARSENAL
BEKI wa Roma, Mgiriki Kostas Manolas, 27, ambaye anawindwa na Arsenal na Manchester United, anahitaji kupata zaidi ya pauni milioni 12.5 kutoka kwa wanaomhitaji kwa kuondoa kipengele kinachomruhusu kuondoka katika mkataba wake. ***(Mirror)***

### SAISS AIPAGAWISHA ATLETICO
KIUNGO wa Wolves, Romain Saiss, 28, anatakiwa na Atletico Madrid, wakati huu klabu hiyo ya La Liga ikiwa tayari kumnasa Mmorocco huyo majira ya joto. ***(Lions de l'Atlas via Birmingham Live)***

### NDOMBELE AIVUTIA UNITED
Manchester United inavutiwa na kiungo wa Lyon, Tanguy Ndombele, 22, wakati huu mchezaji huyo akitakiwa pia na Juventus. ***(Metro)***

### RAKITIC KUISUBIRISHA BARCA
KIUNGO wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 30, atachelewa kuongeza mkataba na miamba hiyo ya Hispania hadi majira ya joto. ***(Marca)***

### SALMAN KUINUNUA UNITED
MTOTO wa Mfalme wa Saudia, Mohammed bin Salman amepiga hatua kuhusu ofa yake ya pauni bilioni 3.8 ya kuinunua Manchester United, akiwa na matumaini ya kuwa mmiliki mpya wa klabu hiyo msimu ujao. ***(Sun)***



HABARI MICHEZO

# MBIO ZA NYIKA ZATOA 28 WA TIMU YA TAIFA

Na Mwandishi Wetu, Moshi

Mashindano ya Taifa ya Mbio za Nyika yaliyofanyika mwishoni mwa wiki mjini moshi, yamefanikisha kupatikana kwa wanariadha 28 watakaounda timu ya Taifa ya Riadha itakayoshiriki mashindano kama hayo ya dunia ambayo yatakayofanyika nchini Denmark mwishoni mwa mwezi ujao.

Katika mashindano hayo yaliyofanyika chini ya udhamini wa DStv na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, yalikuwa katika makundi manne ambapo kundi la kwanza na la pili ni la wanaume na wanawake wa umri wa zaidi ya miaka 18, na la tatu na nne wavulana na wasichana chini ya miaka 18.

Akitangaza timu hiyo ambayo itaweka kambi jijini Arusha, mara baada ya mashindano hayo, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania, Wilhelm Gidabuday, alisema mashindano ya mwaka huu yamekuwa na ufanisi mkubwa kwani yameshirikisha wanariadha wengi na pia kumekuwa na wanariadha wapya ambao wameonyesha uwezo mkubwa.

Aliwatangaza wachezaji watakaokuwa katika kundi la wanaume wenye umri wa zaidi ya miaka 18 kuwa ni Faraja Damas (Arusha), Joseph Panga(Arusha), Sylvester Marco (Arusha), Stephano Huche (Arusha), Deogratius Nade (Manyara), Yohane Elisante (Arusha) na Bazil Sule (Polisi).

Kwa upande wa wanawake katika kundi hilo ni Failuna Abdi (Arusha), Magdalena Shauri (JKT), Anjelina Daniel (Arusha), Amina Mohamed (Arusha), Marselina Issa (Arusha) na Neema Masud (Arusha).

Kundi la wavulana chini ya miaka 18 litakuwa na wachezaji saba ambao ni Michael Kishimba (Arusha), Daniel Sinda (Arusha) Emmanuel Joseph (Manyara) Francis Damiano (Mbulu), Saimon Francis (Arusha) na Nicodemo Joseph (Mbulu) wakati wasichana watakuwa ni Agnes Protus (Arusha), Anastazia Ndoromongo (Arusha), Aisha Luguna (Arusha), Sara Hiti (JKT), Gace Jackson (JKT), Noela Lemmy (Arusha) na Catherine Philipo (Manyara). Kambi hiyo itakuwa chini ya jopo la wataalamu nane wakiongozwa na Kocha wa Riadha, Meta Petro kutoka Klabu ya Riadha ya Rift Valley. wengine ni Anthony Mwingereza (JWTZ), Anrea Panga (JKT), Thomas Tlanka (Arusha) na Juma Jambau (Singida).

Mwanariadha maarufu mstaafu Marcelina Gwandu ameteuliwa kuwa muangalizi (Matron) wa kambi hiyo huku Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Dk. Hamad Ndee akipewa jukumu la kuratibu mafunzo hayo.

Akizungumza muda mfupi baada ya Mashindano hayo, Meneja Uhusiano wa MultiChoice Tanzania (DStv) Johnson Mshana, alisema DStv imekuwa ikishiriki kwa muda mrefu sasa katika kuinua mchezo wa riadha hapa nchini na kwamba ushiriki wao katika kufanikisha mashindano hayo ni katika mkakati wake endelevu wa kuhakikisha kuwa vipaji vya wanariadha wetu vinakuzwa na hatimaye kuweza kuliletea taifa medali katika mashindano ya kimataifa.

"Tuna mkakati kabambe wa 'Ni Zamu Yetu' ambao lengo lake kubwa ni kuhakikisha kuwa wimbo wetu wa Taifa unapigwa katika michuano ya Olimpiki – hii ikimaanisha kuhakikisha kuwa nchi yetu inapata medali katika mashindano hayo makubwa," alisema Mshana na kuongeza kuwa kwa kufanya hivyo pia kutaifanya riadha kuwa moja ya vyanzo vikubwa vya ajira na kipato kwa wanariadha na taifa kwa ujumla huku pia ukiwa ni ulingo mzuri wa kuitangaza nchi yetu kimataifa.



Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya Uzalishaji wa Mvinyo ya Alko Vintages ya jijini Dodoma, Sweetbertha Rwabizi (kulia), akimhudumia mmoja wa wageni waliojitokeza kufurahia pamoja siku ya wapendanao yaani Valentine Day wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# Tamasha la Mkeka na Mvinyo lafana Dar

Na Mwandishi Wetu

HATIMAYE wakazi wa jijini Dar es Salaam wakiwa sambamba na wapendwa wao, mwishoni mwa wiki walipata fursa ya kufurahia pamoja Siku ya Wapendanao ['Valentine Day'] katika hafla maalum iliyofahamika kama 'Mkeka na Mvinyo' na kuvuta hisia kubwa huku waandaaji wakiahidi mambo makubwa Sikukuu ya Pasaka, Msimu wa Sabasaba, na mwisho wa mwaka yaani 'Likizo Time'.

Katika hafla hiyo iliyofanyika Hoteli ya Whitesands jijini Dar es Salaam, ilishuhudiwa wakazi hao wakijitokeza kwa wingi sambamba na wapendwa wao ili kufurahia siku hiyo maalum ambapo pamoja na vinywaji vingine waliweza kufurahia mvinyo wa aina mbalimbali unaozalishwa hapa nchini.

Mbali na burudani nzuri ya muziki laini kutoka kwa msanii Maximilian Rioba maarufu kwa jina la Milian, kivutio kingine kwenye hafla hiyo kilikuwa ni matumizi ya mikeka ambapo baadhi ya washiriki walipata fursa ya kuketi kwenye mikeka iliyoandaliwa sambamba na meza fupi wakipata vinywaji, vyakula huku wakifuatilia burudani ya muziki iliyokuwa inaendelea.

"Hii ni hafla yetu ya kwanza ya Mkeka na Mvinyo kati ya hafla nyingine nyingi za aina hii zitakazofanyika Sikukuu ya Pasaka, Msimu wa Sabasaba, na mwisho wa mwaka yaani 'Likizo Time'. Tunashukuru kuona hafla hii imepokelewa vizuri na wadau na tunawaahidi mambo mazuri zaidi yanakuja kupitia Mkeka na Mvinyo waendelee kutuunga mkono," alisema Caroline Kirwanda, mratibu wa hafla hiyo kutoka Kampuni ya Real PR Solutions (RPR).

Aliwashukuru baadhi ya wadau muhimu katika kufanikisha hafla hiyo kuwa ni pamoja na kampuni ya uzalishaji wa mvinyo ya Alko Vintages ya jijini Dodoma, Hoteli ya Whitesands, Bodi ya Utalii Tanzania, (TTB), GS 1, pamoja na Kampuni ya TSN."

Kirwanda aliongeza kuwa hafla hiyo ni sehemu ya mkakati wa kampuni hiyo utakaozinduliwa hivi karibuni unaolenga kutangaza utalii wa ndani pamoja kuvumbua fursa mbalimbali za kibiashara ndani ya nchini kwa lengo la kukuza uchumi unaofahamika kwa jina la 'Domestic Tourism Promotion Initiative' (DTPI). "Tunahitaji kuhamasisha zaidi matumizi ya bidhaa za ndani ili kukuza uchumi wetu kama taifa," aliongeza Kirwanda.

Kwa upande wake, Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya Alco Vintages , Sweetbertha Rwabizi alisema ushiriki wao kama wazalishaji wa mvinyo wa ndani kwenye hafla hiyo unalenga kuhamasisha zaidi matumizi ya bidhaa hizo kwa kuwa tofauti na kuuza bidhaa zao pia walipata fursa ya kukutana moja kwa moja na watumiaji wa bidhaa hizo na hivyo kupata mrejesho kutoka kwao huku pia wakijenga uelewa zaidi kwa watumiaji kuhusu vinywaji hivyo.

"Iwapo Watanzania watabadilika na kuanza kutumia bidhaa hii ya mvinyo unaozalishwa hapa nchini, inaweza kukuza soko la wakulima kwa zaidi ya asilimia 80 kutokana na bidhaa hii kuzidi kupata watumiaji kadiri siku zinavyokwenda," alisema.

## Coke Studio 2019 kuwatoa wateja

Na Mtapa Wilson

Kampeni ya Coke Studio 2019 inayojumuisha wasanii watano kutoka Tanzania, imeongeza wigo na kuwagusa wananchi ambapo itawazawadia wateja zaidi ya 500,000 wanaotumia bidhaa za Coca-Cola hapa nchini.

Akizungumza katika uzinduzi wa promosheni hiyo mpya itakayodumu kwa majuma 12, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Idara ya Masoko wa Coca Cola nchini Tanzania na Kenya, Nelly Wainaina, alisema katika promosheni hiyo kampuni yao imelenga kuwanufaisha wateja wake kwa zawadi mbalimbali zikiwamo fedha taslimu, runinga na bidhaa za Coca Cola.

"Tukiwa kama kampuni inayojali wateja wake siku zote tumekuwa tukiwashirikisha kwenye mambo yanayowafurahisha. Kutumia Coke studio ni njia nzuri ya kuwawezesha wateja wetu kujishindia zawadi mbalimbali wakati wakiangalia 'shoo' ya muziki wanaoupenda. Kwa kipindi cha wiki 12," alisema Wainaina.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa masoko, wateja wa Coca Cola Kwanza na Bonite watatakiwa kununua kinywaji chochote chenye ujazo wa mililita 350 na mililita 500 wakati wateja wa Nyanza wanaotaka kujishindia zawadi watalazimika kununua vinywaji vyenye ujazo wa mililita 300 na mililita 350.

"Wateja watatakiwa kuangalia chini ya kizibo kama wamejishindia zawadi. Watakaojishindia zawadi watatakiwa kupeleka vizibo kwenye sehemu za mauzo ya rejareja kwa ajili ya kupata zawadi zao, fedha taslimu zitatolewa kwenye sehemu maalum za mauzo ya bidhaa za Coca Cola wakati washindi wa zawadi za runinga watapata zawadi zao kwenye kiwanda kilichopo jirani na wao," alisema. Wainaina alizitaja bidhaa zitakazokuwa kwenye promosheni hiyo ni pamoja na Coca Cola, Fanta, Sprite, Krest, Stoney, Novida na Spaletta na Pinenut zenye kizibo cha njano.

Mwaka huu, Coke Studio Afrika itawashirikisha wasanii watano wenye vipaji kutoka Tanzania ambao ni Faustina Charles 'Nandy', Raymond Mwakyusa 'Rayvanny, Rajab Abdul 'Harmonize' Juma Mussa 'Jux' pamoja na Marianne Medi 'Mimi Mars' ambaye atajiunga na msimu huu wa mwaka 2019 wakati wa mapumziko marefu ikiwa ni fursa nyingine kwa wasanii wanaochipukia kushiriki kwenye 'shoo' hiyo.

Kampuni ya Coca-Cola imekuwa ikiwashirikisha wateja wake kwenye promosheni mbalimbali moja wapo ikiwa Msisimko wa Soka na Coka wakati wa maandalizi ya Kombe la Dunia yaliyofanyika Urusi mwaka jana.

# Michezo

Jumatatu Februari 18, 2019
Nipashe



## Robben: Anfield kunanitesa sana

HABARI UK 30

JUU KWA JUU...



Kipa wa Manchester City, Ederson, akilazimika kutoka langoni na kuruka juu kuzuia wachezaji wa Newport County, waliojazana ndani ya boksi kujaribu kutafuta furaha ya ushindi kwenye mechi ya Kombe la FA, ambayo City ilishinda 4-1 dhidi ya timu hiyo ya League Two England iliyokuwa uwanja wake wa nyumbani. **HABARI UK. 29**

# ZAHERA ATOA SABABU SIMBA KUIUA YANGA

●●●Ni baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 Taifa, afafanua kuwa kilichochangia ni...

**Na Faustine Feliciane**

YANGA imejikuta ikichezea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa mahasimu wao, Simba kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Taifa, na kocha wa timu hiyo, Mwinyi Zahera, hakuwa kimya kwani amefichua sababu ya timu yake kukubali kichapo hicho.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo, Zahera alisema walifungwa mchezo huo kwa sababu Simba walikuwa juu zaidi yao.

Aidha, Zahera alisema mbali na hilo, wachezaji wa Simba mmoja mmoja ni bora zaidi ukilinganisha na wachezaji wake.

"Simba walikuwa na nafasi kubwa ya kushinda mchezo huu kuliko sisi..., tulikuja uwanjani tukijua kabisa tunaenda kupambana na timu bora na yenye wachezaji wa kiwango kikubwa kuliko sisi, tumekubali matokeo, lakini niwapongeze wachezaji wangu kwa namna walivyopambana, Simba walikuwa bora zaidi yetu," alisema Zahera.

Alisema hakuna wa kumlaumu kwa matokeo waliyoyapata kwa kuwa kila mchezaji alipambana kwa nguvu zake, lakini juhudi zao ziligoma kwa wapinzani wao.

"Hata mabadiliko ambayo niliyafanya ni ya kiufundi zaidi..., Ajibu alionekana kuchoka na pia nilitaka kushambulia zaidi," alisema Zahera.

Alisema anawapongeza Simba kwa ushindi walioupata na wao wanaenda kujipanga kwa ajili ya mchezo unaofuata.

"Tunapitia kwenye wakati mgumu, wachezaji wangu wanapambana na wanajitahidi sana..., baada ya mchezo huu tunaangalia mchezo unaofuata," alisema.

Kwa matokeo ya juzi ni kama Simba iliyofikisha pointi 39 baada ya mechi 16, ilirekebisha makosa yao kwenye mchezo wao wa mzunguko wa kwanza dhidi ya Yanga baada ya kubanwa na kutoka suluhu na miamba hiyo ya Jangwani yenye alama 58 kufuatia kucheza jumla ya mechi 24 hadi sasa.

# Aussems: Tulitaka pointi si mabao

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa Simba, Patrick Aussems, amesema ushindi walioupata kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara juzi dhidi ya watani zao, Yanga, walipania zaidi kuongeza pointi na hawakujali idadi ya mabao.

Aussems aliliambia Nipashe jana kuwa hakutaka idadi ya mabao zaidi ya pointi tatu ili kujiweka vizuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Alisema anashangaa watu wanabeza ushindi wa bao 1-0 walioupata bila kujua ni ushindi muhimu kwao na katika msimamo wa ligi hiyo kwa sasa.

"Mlitaka tufunge mabao mangapi? Nawapongeza wachezaji wangu kwa ushindi huu, kikubwa ni pointi tatu muhimu," alisema Aussems.

Aidha, Aussems aliwapongeza Yanga kwa mchezo mzuri na wa ushindani licha ya kufungwa.

"Niwapongeze pia Yanga, wamecheza vizuri sana, mechi ilikuwa ya kiushindani..., lakini nafikiri tulistahiri ushindi na tumeupata," alisema Aussems.

Alisema ushindi walioupata juzi ni kichocheo cha kufanya vema kwenye michezo inayofuata.

Ushindi wa juzi umewafanya Simba kuibuka wababe kwenye msimu huu dhidi ya watani wao hao baada ya kuvuna jumla ya pointi nne kufuatia mzunguko wa kwanza timu hizo kutoka sare tasa.

Kwa matokeo hayo, Simba ambayo itaifuata Afrika Lyon Uwanja wa Shekh Amri Abedi jijini Arusha Jumanne, imefikisha pointi 39 baada ya mechi 16 wakati Yanga ikibaki na alama zake 58 kufuatia kushuka dimbani mara 24.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >